

ALAMA YA MNYAMA

NA MUHURI WA MUNGU ¹



Na tuendeleo kusimama, kwa muda kidogo tu sasa, kwa ajili ya maombi.

² Baba yetu wa Mbinguni, tunashukuru, kweli, kwa ajili ya majaliwa ya kukusanyika pamoja katika Jina la Bwana Yesu. Sasa mbele zetu limewekwa Neno Lako, na, loo, jinsi tunavyolishughulikia Hilo kwa utulivu, Bwana, na kwa uchaji kwa sababu ni Neno la Mungu.

³ Na itakuwa hivyo, iwe ni mapenzi Yako kwamba ninapaswa kujaribu kuelezea somo muhimu sana, usiku wa leo. Nami ninaomba, Baba, ya kwamba Roho Mtakatifu atanipa maneno ya kusema ambayo yatalifaidi kanisa, na—na kwa manufaa ya Ufalme wa Mungu. Tujalie, Bwana. Wewe ni Baba yetu, nasi tunakupenda kwa moyo wetu wote, nasi tunaomba sasa ya kwamba utatubariki.

⁴ Na ninawazia kile ningefanya kama mikononi mwangu, usiku wa leo, katika bi—bilauri, ningekuwa na tone moja tu la Damu ya Bwana Yesu, jinsi ningelishikilia moyoni mwangu! Na ninii tu, loo, karibu ningegopa kupumua. Lakini basi, Baba, machoni Pako, umenikabidhi mikononi mwangu kikuu zaidi, wale walionunuliwa kwa Damu Yako, Kanisa Lako, ulilotoa Damu Yako kwa ajili yake, kuliokoa. Sasa, tusaide, Bwana, tupate kulilisha kundi la Mungu ambalo Roho Mtakatifu amelifanyia waangalizi. Kwa kuwa tunaomba, katika Jina la Yesu. Amina.

⁵ Mwaweza kuketi. Tunamtumainia Bwana Yesu kutuma baraka Zake juu yetu. Ndio kwanza niwe chumbani dakika chache zilizopita, ndipo kitu fulani kikanitikisa. Ni wangapi wanaomjua Raymond Richey? Ameketi kule nyuma chumbani, ndiyo kwanza nimwombee. Naye amejichosha kupita kiasi, na kujifanya kuvurugika na kushikwa na kiharusi; hali mbaya sana, ndugu mpendwa.

⁶ Ule wakati, Ndugu Raymond alikuwa amesimama pale pale jukwaani usiku huo wakati Malaika wa Bwana aliposhuka mbele ya maelfu ya watu wakati niliposema kama...wakati Dk. Best alipokuwa akifanya mjadala kuhusu, pamoja na Dk. Bosworth, kuhusu huduma yangu, nami nikasema, “Sidai kuwa mponyaji.” Nikasema...

Akasema, “Hakuna mtu ila kundi la watakatifu wanaojibingirisha wameamini hilo.”

⁷ Nikasema, “Ni Wabaptisti wangapi hapa, ambao ni wafuasi wa makanisa haya ya Kibaptisti, wanaoweza kusema, na wanaweza kuthibitisha ya kwamba wameponywa na Bwana, inua mkono wako.” Na yapata, loo, nakisia, mia tatu au zaidi wakasimama, nami nikasema, “Na wao je?” Mnaona?

⁸ Na kwa hiyo basi yeye... Nikasema, “Watu wanaamini katika uponyaji wa Kiungu.” Nikasema, “Mimi si—mimi si mponyaji wa Kiungu, kamwe sidai hilo.” Nikasema, “Vitabu vyangu vinachapishwa katika lugha nyingi mbalimbali,” nikasema, “kamwe sikudai kuwa m—mponyaji.” Nikasema, “Ni—ninadai tu kuwa mtumishi wa Mungu.”

⁹ Kisha nikasema, “Sasa, ikiwa karama ya Mungu, ambayo alinipa ya upambanuzi,” nikasema, “sasa, kama hiyo inapigiwa swali, Mungu atajitetea Mwenyewe.” Yapata wakati huo Huyu hapa anashuka, akishuka namna *hiyo*. Hapo ndipo walipopiga picha Yake.

¹⁰ Naye akaniambia, akapiga magoti nyuma kule, baada ya mimi kumwombea, akanikumbatia, akasema, “Nina ujumbe kwa ajili yako.”

“Ati nini?”

¹¹ Kasema, “Acha kuhubiri kwa nguvu sana, na kwa muda mrefu sana.” Akasema, “Utaenda njia ile ile niliyoenda.” Karibu nifanye hivyo wakati mmoja, kwa vyovyote vile. Kasema, “Ndugu Branham,” kasema, “katika hayo maono na kadhalika, ninaona jinsi inavyokufanya.” Kasema, “Niliendelea tu kusonga mbele,” kasema, “nilikuwa na pumziko moja,” kisha akaanza kwenda ng’ambo, akawa na jingine, naye huyo hapo, Mungu asipomgusa, maisha yake yamekwisha.

¹² Kwa hiyo, akasema, “Huwezi kufanya zaidi.” Kasema, “Kutakuwako na wengine watakaosema, ‘*Hili, lile, ama hili, ama lile*, ama kadhalika,’ lakini,” kasema, “hiyo haitaiboresha.” Kasema, “Maadamu unaachilia ninii... unafanya huduma yako, unaonyesha watu ya kwamba Mungu alikutuma,” kasema, “basi hilo latosha, acha tu iende hivyo.” Kasema, “Kama—kama hawataninii,” kasema, “wasiponinii...” Kasema...

¹³ Alinifanya niahidi mle ndani huku mikono yangu ikiwa kwenye yake, kasema, “Usifanye hivyo tena, Ndugu Branham. Kumbuka, nimeonywa na Bwana kukwambia, utagonga mwamba niliogonga,” mnaona, “ukifanya hivyo tena, ukianza kufanya hivyo.”

Nami nikasema, “Sawa, Ndugu.”

¹⁴ Usimwambie mke wangu hilo, anaye Billy, na hao wengine waliomzunguka kila mahali, na Leo, na Gene, na hao wote, kama wakiniona nikiingia uchovu hata kidogo, vema, basi wanapaswa kuniondoa jukwaani, nitake nisitake kuondoka. Na kama angejua ningeyumbayumba jukwaani namna hiyo,

mbona, angekuwa akilia, akiendelea. Kwa hiyo sisi . . . Unaweza tu kufanya *kiasi fulani*, mwajua, wala huwezi kufanya la zaidi, hivyo tu.

¹⁵ Ninakumbuka wakati mmoja Paul Rader . . . Ni wangapi waliowahi kumjua? Hakika, Paul Rader alikuwa mtu mashuhuri wa Mungu. Alisimulia hadithi ndogo wakati mmoja, kasema alikuwa amepanda garimoshi, na akasema alikuwa na mtu mwingine, na kasema mtu huyu alijaribu kumkosoa kwa sababu alilala kwenye behewa la kulala usiku huo. Kasema kwenye kiamshakinywa kesho yake asubuhi, kundi la wahudumu lilikuwa likienda mahali fulani kwa ajili ya mkutano mkubwa, kasema mtu huyu aliketi papo hapo karibu na Paul, na kusema, “Vema, Mungu asifiwe.” Akasema, “*Ahem!* Niliketi kitini kwenye behewa jana usiku,” kisha kasema, “nikamwokolea Bwana pesa.”

¹⁶ Paul akasema, “Mungu asifiwe, nilichukua behewa la kulala nikamwokoa mtu wa Bwana.” Yeye anavutiwa na nini za—zaidi? Pesa Zake ama mtu Wake? Mtu wake, daima. Tuna furaha sana kwa ajili yake.

¹⁷ Na sasa, nilikuwa na wakati mzuri sana jana usiku, niliwazia, mimi mwenyewe. Na mara tu nilipokuwa nikiondoka, ule m—mvuto wa watu, wa Roho Mtakatifu, alishuka moja kwa moja miongoni mwa watu, na kuanza kutoa upambanuzi moja kwa moja mkutanoni. Jinsi hilo lilivyokuwa tukufu! Mnaona, na kwangu mimi, hilo linamfanya kila mtu mkutanoni kuombewa. Mnaona? Mnaona? Sasa, nilisema, “Ni wangapi hapa . . .?”

¹⁸ Sasa, Mungu aliahidi angefanya hivyo. Sasa, hilo ni Neno Lake, sivyo? Sasa, Mungu hutimiza Neno Lake, sivyo? Ndipo nikasema, “Sasa, ni wangapi hapa ambao ni waaminio? Inueni mikono yenu.” Kila mtu aliinua mikono yao. Nikasema, “Sasa, wekeaneni mikono. Sasa, Biblia ilisema, ‘Ishara hizi zitafuatana na hao waaminio.’” Ndipo tukamwomba kila mtu, huo ulikuwa ni mkono uliunganishwa pamoja kwa ajili ya Ufalme wa Mungu. Loo, jamani, kwangu mimi, hilo ni kamilifu kabisa. Mnaona?

¹⁹ Nilikuwa kwenye kituo cha petroli leo, nikinunua petroli, hapa mahali fulani, ndipo maskini jamaa mmoja akatokea, akaniangalia, akasema, “Wewe ni Ndugu Branham!”

Nikasema, “Naam.” Yapata maili moja hapa, ama kadhalika.

²⁰ Naye akasema—kasema, “Mimi ni Ndugu Roberts,” kisha akasema, “mama yangu hakika aliponywa ugonjwa wa moyo tangu umekuwa huko chini kwenye kanisa la Assemblies of God.” Kasema, “Ameshikwa na mafua makali,” kasema, “hajawa na hata chembe moja ya ugonjwa wa moyo tangu alipoitwa,” chochote ulichokuwa, mnaona, hata moja.

²¹ Kisha kasema, “Ana mafua makali,” kisha kasema, “kama akijua ya kwamba nilikutana nawe hapa chini, na ajue

unamwombea,” kasema, “atakuja mkutanoni, usiku wa leo.” Kasema, “Anataka kujaribu kuja huku Jumapili usiku kama akiweza.” Labda yeye ni mfuasi wa kanisa lingine, lakini aliponywa hapa, kwa hiyo tunafurahia hilo.

²² Na kuona shuhuda zikiingia wakati wote wa watu mbalimbali. Nami ninakutana na watu walioponywa huko nyuma katika mwaka wa 1946 na '47 tulipokuwa hapa, huko nyuma kabisa, wangali wanaendelea, hawajapata shida hata kidogo tangu wakati huo.

²³ Kulikuwa na mama fulani mahali fulani, ndiyo kwanza nipate barua yake, ninaamini leo. Ameketi hapa ndani, kanisani nadhani, usiku wa leo. Yeye alikuja. . . Aliponywa hapa nilipokuwa hapa katika mwaka wa '46 ama '7, mahali fulani, akiwa na kansa. Halafu baadaye akaugua uvimbe mkubwa, nao huo uvimbe ulikuwa mkubwa sana hata iliwabidi kumbebabeba kila mahali alipoenda, namna *hii*. Nao ulikuwa mkubwa sana usingefanyiwa upasuaji, kwa hiyo wakamleta Jeffersonville.

²⁴ Nami nilikuwa huko ndani kwenye maskani ndogo kwa usiku mmoja, na wanaume fulani walikuwa wamemketisha kwenye kona, ndipo kasema ya kwamba—ya kwamba mimi. . . Yeye alipitia tu hapa majuma machache yaliyopita na kunionyesha kilichokuwa kimetukia. Naye alikuwa mkubwa sana, hata baadhi ya mashemasi na wadhamini wa kanisa. . . Alitaka kuombewa, na huko maskanini wakati mwingine siwaombe watu zaidi ya kusimama tu Jumapili asubuhi, labda, nikiwa huko; siwi huko mara nyingi sana.

²⁵ Nao wakambebea na kumketisha chini, huko nyuma ya mahali nilipokuwa nikitokea, basi nikipita, ilitokea kwamba Roho Mtakatifu aliangalia kando, akanifanya niangalie kando, ndipo nikamwona, nikamwambia habari zake, nikamwekea mikono, naye ni wa kawaida tu kama mtu mwingine yeyote.

²⁶ Kisha nikapata barua yake. Sijui kama mama huyo yuko hapa usiku wa leo, anaweza kuinua mkono wake? Alikuwa humu kanisani hivi majuzi usiku, yeye na mumewe, wako hapa, naamini. A—alikuja kwa trela, na akasimama nje ya nyumba yangu hivi majuzi tu na—na alikuwa akizungumza nami.

²⁷ Nami ninaamini alisema ya kwamba alikuwa amejifunza kuwa rafiki wa mama ya Ndugu Mercier, ama kitu kama hicho, alikuwa akiniambia katika barua. Nami nilifikiri labda angekuwa hapa. Barua hiyo iliandikwa juma lililopita. Lakini mimi. . . (Ati nini?)

²⁸ Huko upande wa kulia, hao watu wako, ambavyo Ndugu Mercier, ama, Ndugu Goad amesema. Mama huyo yuko sehemu ya kulia yule aliyekuwa na huo uvimbe mkubwa, alikuwa nyumbani na aliponywa. Kama yuko sehemu ya kulia hapo mahali fulani, kwa nini usitoke hapa nje na kuwaacha watu waone kile Mungu anachoweza kumfanyia mtu ambaye kweli—

kweli ameponywa, huku akiwa mkubwa sana ilimbidi kubebwa-bebwa kila mahali. Hiyo ni...? Ati hayuko huko nyuma? Vema, hapana shaka wametoka hivi punde. Ndugu Goad alisema walikuwa wameketi pale muda mfupi uliopita. Ukiwaangalia, ningetaka yeye atoe huo ushuhuda.

Mwembamba tu kama nilivyo mimi, naye alikuwa tu *hivi*, uh-huh, akiwa na uvimbe. Na jinsi Bwana... Kama tungeninii tu...

²⁹ Sasa, angalieni, sasa nilisema nini kumhusu Mungu? Ataku-... Kama mtu mwingine aliye na uvimbe mkubwa hivi, atatenda vile vile alivyotenda, Mungu hana budi kutenda vile, vile vile kwako kama Yeye alivyomtendea. Kama hakufanya hivyo, alifa-... Alifanya makosa alipomponya. Mnaona? Mungu hawezi kukosea, kwa hiyo yale anayomtendea mmoja, hana budi kumtendea huyo mwingine. Sasa, kuna sharti moja tu: Kama utatumia tu imani ile ile rahisi, hivyo tu.

³⁰ Maskini mwanamke mmoja hapa juu mahali fulani mahali panapoitwa *Eureka*, ninaamini hapo ni Eureka, California, nilishuka nikaja miaka mingi iliyopita wala sijapata kumwona mtu yeyote...hata wasingeweza kumtoa kitandani. Vema, maskini kichwa chake, mahali alipokuwa amevimba, samahani hili dada zangu, tafadhalini, titi la huyo mwanamke lilikuwa limetokeza moja kwa moja namna *hii*, mnaona, kutoka mahali alipokuwa amevimba kwa uvimbe huu. Naye mumewe aliendesha tekisi.

Nami nikasema, “Ndugu, sioni jinsi...” Imani yangu hata ilipungua yenyewe nilipomwangalia huyo. Nami nikasema, “Hivi umekuwa na daktari?”

Kasema, “Hatuamini kuwa na madaktari.”

Kasema, “Vema, sawa.”

Kasema, “Kama akifa, afe, bali tunamtumainia Mungu.”

Nikasema, “Vema, hiyo kweli ni imani.”

Kasema, “Jambo pekee ninalotaka ufanye ni kuingia mle na kuweka mikono yako juu ya mke wangu na kumwombea, Ndugu Branham, naye ataponywa.”

³¹ Loo, jamani! I—itabidi nikubali alikuwa na imani nyingi kidogo kuliko niliyokuwa nayo, hiyo ni kweli. Nilikuwa tu nimeanza huduma, nilikuwa na yapata mwaka mmoja, sikuwa nimeona kitu kama hicho kimefanywa bado. Basi nikaenda na kumwekea mikono mwanamke huyo, na mnajua nini?

³² Sasa, hii ni hadithi yake kwenye barua, huenda yuko papa hapa sasa, ubavu wake ulipasuka, na galoni za maji zikabubujika kutoka kwake. Likapona moja kwa moja tena, naye ni, yapata, kufikia yapata ratili mia moja na kitu, ratili mia na tano, kumi. Yeye hafanyi tu kazi yake mwenyewe, bali anafanya kazi zote za majirani. Kwa hiyo, anaenda moja kwa

moja huku na huko mtaani, anaenda na kuwatunza watoto wao, kuwafulia na mambo kama hayo. Anaenda tu . . .

³³ Sasa, kama mtu yule yule, mtu mwingine, akikaribia kwa msingi uo huo, Yeye hana budi kufanya jambo lile lile, ama kama hakulifanya, basi Yeye alikosea. Alikosea basi alipomponya huyo—huyo mwanamke mmoja, na kumponya hivyo, basi alikosea wakati Yeye—wakati Yeye alipomponya, kama Yeye—kama Yeye ha- . . . kama Yeye hakufanya . . .

³⁴ Kama Yeye—kama Yeye alimponya, basi asipokuponya, Yeye alikosea basi wakati alipomponya wa kwanza, endapo utatimiza masharti yale yale ya imani aliyotimiza. Inategemea tu jambo moja, “Ninaweza kama ukiamini.” Hivyo tu. Kwa hiyo, mnaona, basi yote yanategemea, haidhuru tunatilia mkazo kiasi gani, ama tunaweka nini juu yake, si hivyo, ni kutulia na kuamini. Useme, “Mimi . . .”

³⁵ Mimi huyo hapo ninaenda tena, Ndugu Roy. Unaona? Hivi ulinisomea Maandiko? Nimeombwa kuzungumza juu ya somo, ama nilisema mwenyewe ya kwamba ningelizungumzia, hasa, juu ya somo la *Alama Ya Mnyama Na Muhuri Wa Mungu*. Sasa, ni somo kuu. Nami nafikiri ya kwamba huenda tusilimalizie usiku wa leo, labda itatubidi kuliendeleza mpaka kesho usiku.

³⁶ Na wale walio na mahojiano sasa, naamini Bw. Mercier alisema tulipaswa kuanza saa mbili asubuhi. Sasa, nina mahojiano ya kibinafsi ambapo watu wanataka kuona kwa ajili ya maono, na kadhalika. Hapo ndipo ninyi nyote hamlipati, mnaona, hapa, ni siku nzima, pia, mnaona, halafu, kwenye mahojiano haya ya kibinafsi. Kwa hiyo sasa kumbukeni, mimi . . . yeyote aliye wa kwanza asubuhi, yanaanza saa mbili. Sasa, aliniambia tu dakika chache zilizopita.

³⁷ Sasa, juu ya somo hili kuu la *Alama Ya Mnyama Na Muhuri Wa Mungu*, tumesikia mengi sana kulihusu. Limekuwa . . . Nimeona chati ambazo zingefunika jukwaa hili hapa kuhusu “Alama Ya Mnyama, Muhuri Wa Mungu.” Lakini kwangu mimi, ni rahisi sana, ni ja—jambo rahisi sana kuangalia katika Neno na kuliona, mpaka sidhani . . . Vema, nina yapata kurasa tatu ama nne za Maandiko mbalimbali ninayotaka, yaliyoandikwa hapa, ambayo ninataka kuyarejea usiku wa leo. Nilipokuwa nikiliwazia alasiri ya leo, niliandika Maandiko hapa, na kurasa mbalimbali, kusudi nipate kujua, nanyi mngeweza kuliandika mkitaka.

³⁸ Sasa, ni somo kuu, nami nafikiri kwamba ni . . . na moja ya ninii . . . somo muhimu linalopaswa kufundishwa. Sasa, tumekuwa na mahubiri ya Injili, tumekuwa na uponyaji wa Kiungu. Na sasa, hili linapaswa kuwa ninii . . . kwenye msingi, kama vile, Kuja kwa pili kwa Kristo, katika Kuja Kwake mara ya pili.

39 Ndugu Smith, huyo ni mke wako? Vema mimi... U hali gani, Dada Smith? Mimi—mimi... Si ajabu yeye ni—yeye ni mtu mzuri, wewe ni maskini mama mwenye sura nzuri, anayeonekana mtauwa, kama mke. Huenda ni—nimekutana nawe hapo awali. Wanasema nyuma ya kila mwanamume mwema kuna mke mwema. Hilo—hilo ni sawa kabisa.

40 Ninajua mke wangu ni... Kama kuna sifa yoyote ya kuiendea familia ya Branham, mpeni yeye, kwa sababu yeye ndiye ambaye... Lakini yeye ana umri mdogo kuliko mimi kwa miaka kumi na ana kichwa cheupe kama theluji, naye yuko hivyo, kwa sababu tu amesimama kati yangu na umma, wala sijui ningefanya nini bila yeye. Mungu hakika alinipa mke mzuri sana.

41 Wao ni kitu cha ajabu, Ndugu Smith. Ninii tu, mbona, kama angaliweza kumpa mtu chochote kilicho bora zaidi, angalifanya hivyo. Hiyo ni kweli. Sawa. Hiyo ni kweli. Huo ndio ukweli. “Apataye mke, amepata kitu chema,” asema mtu mwenye hekima kuliko wote tuliyepata kuwa naye. Na—nafikiri ya kwamba mke ndicho kitu kizuri sana mwanamume awezacho kuwa nacho nje ya wokovu. Hiyo ni kweli, hiyo ni kweli, anapendeza.

42 Sasa, nitawekea msingi Maandiko hayo... Kwanza nitawaambia kile ninawazia ndicho alama ya mnyama, na kile, nafikiri Maandiko yanaunga mkono alama ya mnyama kuwa, kisha nitawaambia kile ninachowazia Maandiko yanaunga mkono Muhuri wa Mungu kuwa.

43 Sasa, tunajua ya kwamba mambo haya mawili makuu yanaishia hivi karibuni katika mishiko miwili mikuu, mikuu zaidi. Ulimwengu umeshikwa na vitu hivi viwili sasa hivi, alama ya mnyama, ama Muhuri wa Mungu. Baadhi yao wanaliweka huko mbali sana katika siku za usoni, wengine wanasema tayari imekuwa katika wakati uliopita. Lakini ninaamini ya kwamba kuna majibu mawili tu kwake, na hiyo ni kwamba Muhuri wa Mungu ni ubatizo wa Roho Mtakatifu, alama ya mnyama ni kuukataa. Sasa, hayo ndiyo mambo mawili pekee, nitawapa Maandiko ni kwa nini sasa, tunapoendelea.

44 Sasa, mmoja wao ni, kumbukeni, watu wote duniani katika siku za mwisho ama watatiwa muhuri kwa Muhuri wa Mungu, ama kutiwa alama kwa alama ya mnyama.

45 “Naye aliwafanya wote, maskini, wakubwa, watumwa, walio huru, wote duniani kupokea alama hii ambao hawakuwa na Muhuri, na ambao majina yao hayakuandikwa katika Kitabu cha Uzima cha Mwana-Kondoo tangu kuwekwa misingi ya ulimwengu.”

46 “Tangu kuwekwa misingi ya ulimwengu,” wakati Mwana-Kondoo alipochinjwa, ndipo majina yao yalipoandikwa kwenye

Kitabu cha Uzima cha Mwana-Kondoo, sasa, hivyo vitu viwili vikuu.

⁴⁷ Sasa, kwanza tutaanzia juu ya *Muhuri Wa Mungu*. Sasa, muhuri ni nini? Kwanza, muhuri katika Biblia, huko nyuma siku nyingi kabla watu kuwa, wameelimika, kama walivyo sasa, wao kwa kawaida, muhuri wao ulikuwa ndio sahihi yao kama tu tunavyoitumia siku hizi kama jina letu. Wakati mwingine Warumi, na huko nyuma katika Wayahudi, na huko nyuma kabisa katika nchi za mashariki za mwanzoni, wangekuwa na pete, iliyokuwa na muhuri wao, *hah*, na kuupigia juu ya kitu fulani. [Ndugu Branham aliiga kupiga muhuri—Mh.] Kama wasingeweza kuandika jina lao, muhuri huo.

⁴⁸ Muhuri ulikuwa ni thibitisho halisi, ambalo lilitiwa muhuri kwa muhuri huu. Na ku—kujaribu kunakili huu, ilikuwa ni adhabu ya kifo, kama tu vile ingekuwa sasa kujaribu kughushi hundi, jina la mtu fulani kwenye hundi, ilikuwa ni fa—faini kubwa kujaribu kunakili muhuri huu. Na kwa kawaida mtu aliyeivaa, aliyekuwa na muhuri wake, aliuvaa nyuma ya kifundo cha mkono wake, ama—ama kwenye pete yake. Naye angeitia muhuri badala ya kuandika jina lake, hiyo ilikuwa ni kuonyesha ya kwamba—ya kwamba ilikuwa, alikuwa ameitia muhuri.

⁴⁹ Sasa, sasa, Yesu alisema ya kwamba katika siku za mwisho, kulingana na Mathayo Mtakatifu mlango wa 24 na kifungu cha 24, ya kwamba roho hizi mbili, hizi, wale waliotiwa muhuri na Mungu, na wale ambao wangetiwa alama na yule mnyama, mpinga-Kristo, wangepanana sana hata ingewapoteza walio Wateule kama yamkini, mnaona. Sasa, watafanana sana.

Sasa, watu wengine husema, “Vema, ukomunisti ndio alama ya mnyama.”

⁵⁰ Umekosea, ukomunisti sio alama ya mnyama, hata hivyo ndio, bali hauelekei huko. A—alama ya mnyama ni—ni asili ya kidini, ya kidini sana, mwenye hila na mjanja sana, mpaka itawapoteza walio Wateule kama yamkini, zinafanana sana hata zingewapoteza walio Wateule kama yamkini. Bila shaka, wao . . .

⁵¹ Billy Graham alisema si muda mrefu uliopita, nilikuwa nikimsikiliza Jumapili chache zilizopita kwenye redio yangu nikishuka kuja huku, naye alikuwa akihubiri, akasema, “Mnasikia mengi sana kuhusu sigara, na Viceroy,” ama chochote kilichokuwa, na “ncha kwenye mwisho *huu*, na moto kwenye mwisho *huu*, na kila kitu namna hiyo,” kasema, “mtu ambaye angezivuta kwa vovyote vile alikuwa ni mpumbavu.” Nami nafikiri karibu yuko sahihi. Kasema ya kwamba “Hata zilitangazwa sana kwenye vitu kama hivyo, mpaka ibilisi alikuwa amewadanganya Wateule.”

⁵² Si—siamini Ndugu Graham alilimaanisha tu hivyo, kwa sababu Wateule hawatadanganywa. La, bwana, hawatadanganywa, walichaguliwa tangu zamani na Mungu,

nao hawatadanganywa. Kwa hiyo, lakini Yesu alisema ya kwamba wangepanana sana, wangepanana sana, sasa kumbukeni, ya kwamba wangepanana sana hata walio Wateule wangedanganyika kama yamkini.

⁵³ Sasa, tunataka kujua yalikotoka. Haya yote yalianzia wapi? Kama nilivyowaambia ya kwamba kila dhehebu na kila dini ilianzia katika Mwanzo, kila kitu tulicho nacho. Assemblies of God ilianzia katika Mwanzo, Baptisti ilianzia katika Mwanzo, ninaweza kuthibitisha hilo. Naam, bwana. Kila dini potovu, hata, tuliyo nayo, ninaweza kuthibitisha, ilianzia katika Mwanzo. Hiyo ni kweli. Kichunguzeni tu Mwanzo, kisha uende ukachunguze hayo mengine, uone ni mbegu ya namna gani, uone inakoelekea. Mnaona? Basi uiangalie tu, nayo itajipenyeza moja kwa moja kote katika Biblia, vivyo hivyo hasa. Zote mbili zilianzia katika Mwanzo. Nasi tunaona ya kwamba Mwanzo ni mlango wa mbegu.

⁵⁴ Sasa, tunaona ya kwamba kutiwa alama kwa kwanza kwa mwanadamu kulianzia katika Mwanzo, Mwanzo 4:15, Mungu alimtia Kaini alama. Hapo ndipo alama ya kwanza ya mnyama ilipopata kuwekwa, iliwekwa juu ya Kaini, yeye ndiye mwanzo wake.

Sasa, mnasema, “Ati Kaini kuwa na alama ya mnyama?”

⁵⁵ Vema, hebu tuone, sasa, Yeye alisema, “Uzao wako utakiponda kichwa cha nyoka, nacho kichwa chake kitakuponda kisigino.” Angalieni ukoo wa Kaini, wakati Kaini akishuka, walikuwa wanasayansi, watu werevu, watu mashuhuri, na kuendelea namna hiyo. Lakini uzao wa Sethi wakati ukishuka, ukawa wakulima wadogo, wachunga kondoo, wakulima. Kwa hiyo, mnaona, kuna... Sasa, angalieni, Biblia ilisema, “Nitaweka uadui,” Mungu alisema, “kati ya uzao wako na uzao wa nyoka.” Sasa, kwa hiyo...

⁵⁶ Sasa, ndugu wahudumu, tulieni tu kwa dakika moja tu, na— najua daima wanashukia shingoni mwangu juu ya hili. Lakini Biblia ilisema ya kwamba yule nyoka alikuwa na uzao, hilo latosha. Uzao wa nyoka, hebu uwe kwa njia yoyote unayotaka kuuchukua, tutajizua kuingilia huo; nina wazo langu, pia. Lakini wao... Lakini, hata uwe chochote utakachokuwa, Biblia ilisema katika Mwanzo 1, kwamba, Mwanzo moja, ya kwamba nyoka alikuwa na uzao.

⁵⁷ Na sasa kumbukeni, kwanza kabisa huyo nyoka hakuwa nyoka mtambaachi, mtambaazi, alikuwa kiumbe cha pili kutoka kwa mwanadamu. Sayansi imejaribu kwa maelfu ya miaka kupata kiungo kile kilichopotea kati ya mwanadamu na mnyama, kile kilicho karibu sana wanachoweza kufikia ni sokwe mtu, bali hawawezi kupata kile kilicho kati ya sokwe mtu na mwanadamu. Kwa nini? Kilikuwa ni yule nyoka.

⁵⁸ Sasa, ukiangalia katika Mwanzo 3:1, “Mnyama...Nyoka alikuwa mwerevu kuliko wanyama wote wa mwitu.” Mnyama, si mtambaaji. Alikuwa anafanana sana na mwanadamu, alionekana kama mwanadamu, alikuwa ndiye kiungo kile kilichopotelea hapo katikati, kwa sababu hiyo ndiyo njia pekee. Uzao wa mwanadamu hautaingiana na uzao wa mnyama. Lakini jamaa huyu ndiye pekee ibilisi angeweza kumtumia, kwa sababu alikuwa tu kati ya mwanadamu na mnyama. Katika koo...

⁵⁹ Ninaamini katika mageuzo yanayoendelea. Jambo la kwanza labda, wakati hakukuwa na kitu ila machafuko dhahiri tu, mlipuko wa volkeno...Mwajua, Mungu ni Mkandarasi hodari. Mnaamini hilo? Mkandarasi mkuu daima huweka vitu vyake vyote anapojenga mgawo wake. Mungu, wakati alipokuwa akiizunguka dunia, akiumba kalisi, potashi, na petroli, na kadhalika, alikuwa akiweka miili yetu duniani papo hapo, nyenzo tulizofanywa kwazo.

⁶⁰ Ndipo Roho Mtakatifu mkuu akatoka kwa Mungu akaatamia juu ya nchi, ama kunong’oneza, kufanya mapenzi, kama kuku, vifaranga vyake. Na ninii Yake, hebu tuwazie Yeye alikuwa na mabawa, hakuwa nayo, lakini hebu tuwazie Yeye alikuwa na mabawa, kama—kama kuku juu ya vifaranga vyake, akaanza kuatamia juu ya nchi. Nami ninaweza kuona kalisi fulani ikija, ikitiririka mahali padogo, ikichanganyikana na unyevu kidogo na potashi, ndipo ua dogo la Pasaka likachipuka. Nami ninaweza kumsikia akisema, “Njoo hapa, Baba, angalia hili.”

“Vizuri sana. Endelea kuatamia.”

⁶¹ Baada ya kitambo kidogo, akaatamia zaidi kidogo. Kilichofuata labda kilikuwa ni ma—maua na mimea, nao ndege wakaruka kutoka kwenye mavumbi ya nchi, ndipo ukaja uhai wa wanyama, na kuendelea kutokea uhai wa hali ya juu zaidi, uhai wa hali ya juu zaidi, uhai wa hali ya juu zaidi, mpaka hatimaye mtu akatokea katika sura yenyewe ya Mungu. Ajabu ni kwamba hakuna kitu kilichopanda juu zaidi ya hapo, sivyo? Huwezi kwenda juu zaidi, ilikuwa ni sura ya Mungu.

⁶² Kwa hiyo wakati, mageuzo yanayoendelea huileta namna hiyo, ila hawawezi kuchanganya mbegu na kujifanya wa hali ya juu zaidi, Mungu alisema kila mbegu ize kwa jinsi yake. Sasa, katika hilo anakuja basi, mwanadamu.

⁶³ Sasa, dhambi haikuanzia duniani, ilianzia Mbinguni, naye alifukuzwa Mbinguni akaja duniani. Hakuna kitu kingine angaliweza kukiingia, mnyama angekuwa mbali sana naye, mbegu hazingechanganyikana, kwa hiyo ilimbidi kuingia ndani ya huyo nyoka ambaye alikuwa kiumbe kilichofanana sana na mwanadamu.

⁶⁴ Ndipo Mungu alipomlaani na kumweka juu ya tumbo lake, Yeye akabadilisha kila mfupa ndani yake. Sayansi inajaribu kuchimbua mifupa, na, mbona, imefichwa katika siri za Mungu, na itafunuliwa mtu yeyote anayetaka kujua habari zake, hakika. Kuna ninii . . .

⁶⁵ Sasa, angalieni, yeye alikuwa ndiye mjanja kuliko wote, mwerevu kuliko wote, mjanja, mwenye hekima, mwerevu kuliko mnyama, alikuwa karibu kabisa na mwanadamu, mnaona, mjanja kuliko wanyama wote wa mwituni. Na sasa, kumbukeni ya kwamba Kaini alipewa alama. Na sasa, mnasema, “Shetani asingeweza kuwa ndani ya huyo nyoka.”

⁶⁶ Kama mtaenda pamoja nami sasa kwenye Wakorintho wa Pili 11:14, Biblia ilisema alijigeuza akawa kama malaika wa nuru. Mnamchukulia tu kiwepesi Shetani, hivyo tu. Unaona? Naam, bwana. Alijifanya kuwa malaika wa nuru. Angeweza kuja katika kitu cha namna hiyo, basi kwa nini asingeweza kumwingia mnyama, kitu kinachofuata mwanadamu?

⁶⁷ Sasa, tunaona ya kwamba kwa sababu Kaini alimsikiliza adui, basi ilikuwaje? Akawa mwuaji wa kwanza, akawa wa kwanza aliyekuwa na wivu duniani. Niambie ambapo, huo mkondo safi kutoka kwa Mungu hadi kwa Adamu, huo ndio uhusiano wa pekee, Adamu alikuwa ni mwana wa Mungu, Biblia ilisema hivyo, basi huo wivu ulitoka wapi? Huyo mwuaji alitoka wapi? Roho ya aina hiyo yote ilitoka wapi? Kutoka kwa Adamu? Isingewezekana. Ilitoka kwa Shetani, ndiko ilikotoka hasa.

⁶⁸ Sasa, tunaona ya kwamba yeye alikuwa ndiye mwuaji wa kwanza, naye alikuwa ndiye wa kwanza kushikwa na wivu, kama vile Lusifa alivyomwonea wivu Mikaeli, aliuleta moja kwa moja duniani na kuuhamishia kwa mwanadamu. Naye Shetani . . . Kaini kwa kuchukua uovu huu, alichukua alama ya kwanza. Mungu alimtia alama, hakuna mtu aliyepaswa kumwua, achana naye. Lakini mnakumbuka, yeye, mara alipomia alama, alitoka Uweponi mwa Mungu; shikilieni hilo sasa.

⁶⁹ Loo, hatuna wakati wa kulichunguza kwa makini sana kwa sababu, loo, ndugu, tungeweza kuchambua hili hapa kwa muda wa miezi sita, mnaona, pasipo kugusa upande wake wa nje. Mnaona?

⁷⁰ Angalieni, alitoka katika Uwepo wa Mungu wakati alipotiwa alama, akaenda kwenye nchi ya Nodi, na kujichukulia mke. Mfano halisi wa kanisa, linatoka kwa Mungu, linachukua mke wa ulimwengu. Mnaona? Liangalieni. Tukufu! Sasa, itatubidi tubadilishe upesi sasa, tusije tukachukua muda mwingi sana.

⁷¹ Sasa, tunaona ya kwamba basi Habili, ndugu ya Kaini, Kaini alimwua Habili, ndipo Mungu akampa Adamu mwana mwingine badala ya Habili, ambaye jina lake lilikuwa Sethi. Na ilikuwa ni

ishara, na ishara kutoka kwa Mungu ya mauti na ufufuo. Kwa hiyo, Sethi kamwe hakwenda katika nchi ya Nodi kumchukua mke wake, Mungu alimpa mke, lakini Kaini, akiwa na alama ya mnyama juu yake, alitoka akaenda akajitwalia mke katika nchi ya Nodi, naye Sethi akachukua chaguo la Mungu. Mfano mkamilifu wa kanisa la kimadhehebu siku hizi, likitoka nje, likiingiza chochote; bali Kanisa la kweli la Mungu aliye hai, Mwili wa Kristo, huchukua tu kile kilichotiwa muhuri na Roho Mtakatifu, kikamilifu. Mungu ameweka Kanisani.

⁷² Hiyo ishara ilitokana na nini? Makanisa yalitia alama kwa kitu gani? Ishara hii ilikuwa ni nini? Tunajua Kaini alikuwa na ile alama, basi hiyo ishara ilikuwa ni ya nini? Ya ufufuo. Hiyo ndiyo Kanisa limetiwa ishara kwake siku hizi, ishara ya Roho Mtakatifu kwamba Kristo hajafa, bali alifufuka katika wafu na kuingizwa Kanisani. Mnaona, kutia Kanisa Lake muhuri, hiyo hapo inanza moja kwa moja na hao wavulana wawili—wawili, papo hapo katika bustani ya Edeni, moja kwa moja nje ya bustani.

⁷³ Alama ya mnyama: mzururaji, mtoro, hajui anakoenda, hajui mahali ambapo yeye... ambapo yeye... anachojua, hajui anachotaka, yeye ni mtoro.

⁷⁴ Lakini Sethi alikaa nyumbani, naye alikuwa pamoja na baba yake, ndipo Mungu akampa mke, hapo unaanza katika ukoo. Na kama unataka kulifuatilia hilo wakati mmoja... Afadhali niachane nalo. Ninapenda tu kuwathibitishia tena, na tena, na tena, na tena. Naam, bwana. Hiyo ni kweli, hapo ndipo ulipoanzia.

⁷⁵ Baadhi ya watu wanafikiri ya kwamba walikula matofaa katika bustani ya Edeni, wakala matofaa, ndipo muda si muda mwajua, hiyo ilikuwa ndiyo dhambi ya kwanza. Loo, ndugu, hebu nikwambie, sisemi hili kwa mzaha, si mahali pa kufanyia mzaha, lakini kama kula matofaa kutawafanya wanawake watambue kwamba wako uchi, afadhali tuyasambaze hayo matofaa tena, nafikiri hivyo. Nafikiri tunapaswa kufanya hivyo. Haikuwa ni matofaa, sote tunajua hilo. La, tunatambua, katika kusanyiko lililochanganyikana, ilikuwa ni kitu gani, na tunaona kilichofanya.

⁷⁶ Sasa, tunaona basi ya kwamba hii ilikuwa... alama ni utofautishaji, inaonyesha tofauti, inatenganisha kitu fulani. Lakini kama, mnasema, una alama moja dhidi yako, alama, lakini kamwe hukusema ulikuwa na muhuri mmoja dhidi yako, una alama moja dhidi yako. Na muhuri ni ishara ya umilikaji, alama ni utofautishaji. Nalo Kanisa limetiwa muhuri na Roho Mtakatifu, likionyesha kama umilikaji, Mungu analimiliki Kanisa. Lakini alama ya mnyama ni mkaidi, aliyetengwa na jamii aliyekataa kuchukua na kupitia njia ya Mungu iliyoandaliwa.

⁷⁷ Kaini, mara alipotiwa alama, alifukuzwa, tunapata jambo hilo. Habili alikufa, naye Sethi akainuliwa apate kupachukua mahali pake, ilikuwa ni ishara ya ufufuo. Vema.

⁷⁸ Tunaona ya kwamba alama hizi mbili, alama na muhuri zilianza katika Mwanzo, na zinaendelea kote katika Biblia na kuishia katika Ufunuo. Pia tuna Maandiko hapa kuhusu jambo hilo, ambapo lilianzia katika Mwanzo, linaishia katika Ufunuo, daima imekuwa katika namna moja ama nyingine, ikija.

⁷⁹ Kama vile nilivyokuwa nikihubiri hivi majuzi usiku juu ya sadaka ya damu, dhabihu ya damu. Babeli imenenwa katika Mwanzo, mwanzoni mwa Biblia, Babeli ilinenwa katikati ya Biblia, Babeli ilinenwa mwishoni mwa Biblia. Inanzia katika Mwanzo, inakuja kwenye Ufunuo. Kila kitu kinaanza, hizo roho mbili. . .

⁸⁰ Angalieni hapa, sisi, hebu na tulichukue tu kwa dakika moja, hata ndani ya safina, kulikuwako na hua na kunguru ndani ya safina. Mmoja. . . Hao ndege wote wawili, wote wawili wangeweza kuruka, wote wawili. . .

⁸¹ Mnajua kunguru ni mnafiki, yeye ni mnafiki, yeye ni mnafiki mchafu tu. Sasa, kunguru anaweza kuketi chini pale juu ya maskini mzoga wa farasi, na kula tu, na kuwika, na kupigapiga mabawa yake, na kuwa na wakati mzuri sana. Maskini hua huyo hawezi kuukaribia. Kwa nini? Hana nyongo yoyote, mnaona, asingeweza kuumeng'anya. Kama angekula huo angekufa. Lakini kunguru anaweza kuketi hapo na kula mzoga wa farasi nusu siku, aende kondeni kisha arudi nyumbani na kula chakula cha kutwa pamoja na ngano, pamoja na kunguru. . . pamoja na hua. Yeye ni maskini mnafiki, hivyo tu.

⁸² Hivi ulipata kuona, hua hana nyongo ya uchungu; wala mtu yeyote aliyebatizwa kwa Roho Mtakatifu, uchungu wote umekwisha. Wote wawili walikuwa katika safina ile ile, kama vile mnafiki na mwaminio halisi walivyo katika kanisa lile lile, dhehebu lile lile wameketi pamoja, kiti, benchi moja, wameketi pamoja.

⁸³ Ninawatakeni mwone jambo lingine. Loo, ninapenda kuzungumza juu ya maumbile! Hua, hivi ulijua humpati hua akioga. Kwa nini? Haimlazimu kuoga, ana mafuta ndani yake yanayopitia kwenye manyoya yake, naye hujiweka safi wakati wote. Hivyo ndivyo lilivyo Kanisa halisi, si lazima liwe linaoga na kurudi nyuma kuhusu *hili, lile*, ama *linginelo*, bali wanayo Mafuta, Mafuta matakatifu ndani, kila mwaminio, yanayomdumisha akiwa safi mbali na mambo ya ulimwengu.

⁸⁴ Loo, laiti tungeweza tu kuhubiri juu ya—ya Mwana-kondoo na Hua wakati mwingine! Roho Mtakatifu ndani ya mwaminio humdumisha safi, si kile anachoosha kutoka nje, bali hutoka ndani kuja nje. Amina.

⁸⁵ Watu wengi husema, “Sina budi kwenda, kufanya maungamo leo, sina budi kusema *hivi-na-vile*, nami sina budi kwenda kukiri, sina budi kufanya hili.”

⁸⁶ Lakini mnajua, Roho Mtakatifu aliye ndani hutoa tu Mafuta wakati wote, upatanisho, akimdumisha mwaminio safi. “Kwa maana sasa basi, hakuna hukumu ya adhabu juu yao walio katika Kristo Yesu, wasioenenda kwa kufuata mambo ya mwili, bali mambo ya Roho.”

⁸⁷ Tunaingiaje ndani yake? Kwa kupeana mkono kumoja? La. Kwa karatasi moja? Kwa dhehebu moja? La. “Lakini kwa Roho mmoja sote tumebatizwa kuwa Mwili mmoja,” huru na hukumu. Mungu tayari amehukumu Mwili huo, Mungu alihukumu pale Kalvari, haitabidi uhukumiwe tena.

⁸⁸ “Yeye alisikiaye Neno Langu, amwaminiye Yeye aliyenipeleka, yuna Uzima wa Milele,” hakuna aina mbili za Uzima wa Milele, moja tu, “yuna Uzima wa Milele, wala hataingia Hukumuni, bali amepita kutoka mautini kuingia Uzimani.” “Nionapo Damu nitapita, nitapita juu yenu.” Loo, jamani, hilo linanifanya nijisikie kubarikiwa!

⁸⁹ Kwa nini? Huru na dhambi. Hiyo ni kweli. Yeye aliyezaliwa na Mungu hatendi dhambi, hawezi kutenda dhambi, Mbegu ya Mungu inakaa ndani yake, hawezi kutenda dhambi. Haiwezi kuwa ni mimi chini ya dhabihu ya dhambi wakati wote, halafu niwe mwenye dhambi, huwezi. Hujawahi kumwona mwenye dhambi-mtakatifu, hujawahi kumwona ndege mweusi-mweupe, mlevi-asiye mlevi. La, bwana. Ama wewe ni mwenye dhambi, au ni mtakatifu, hivyo tu. Na kama uko ndani ya Kristo, kuna sadaka ya upatanisho wa Damu siku nzima, inayolia, “Baba wasamehe, hawajui watendalo.” Loo, basi unaweza kuwa na uhakika. Amina, napenda hilo. Ni nzuri sana pale, Roho Mtakatifu, jinsi anavyotutia muhuri.

⁹⁰ Angalieni, kunguru, hua, hebu tuone kutoka kwa Kaini na Habili, hao kamwe hawakuwa kitu chochote ila Yuda na Yesu. Bila shaka. Hebu tuuangalie huo moshi. Kama vile Kaini alivyomwua Habili madhabahuni... Sasa Kaini, kama haki ndiyo yote Mungu anayohitaji, ama, kuwa wa kimsingi...

⁹¹ Hivyo ndivyo nilivyosema daima kuhusu hayo matabaka mawili ya watu, ninakutana na wa kimsingi na wa Kipentekoste. Wa kimsingi waliona mahali pao kwa kufundishwa shuleni, wanajua mahali wanaposimama, bali hawana imani; Wapentekoste wanayo imani, bali hawajui wao ni akina nani. Mnaona? Kama nilivyosema, mtu fulani ana pesa kwenye benki, hawezi kuandika hundi, mwingine, anaandika hundi, hana pesa kwenye benki, walete pamoja.

⁹² Sasa, tunaona ya kwamba Wapentekoste ndio walio na imani, wanaamini, lakini, wamejaa Moto, wamejaa Roho Mtakatifu, bali hawajui jinsi ya kutulia kwenye Neno hilo, na

kusema, “Ni BWANA ASEMA HIVI.” Wanayalipua yote kwa filimbi na mayowe, na kupaza sauti, na kukimbia-kimbia. Kama wangaliweza kuyatuliza kabisa, mngeona kanisa likisimama kwa miguu yake katika nguvu na utukufu, kungekuwa na Kitabu cha Matendo kilichoandikwa nyuma yake.

⁹³ Sasa, angalieni. . . Naam, sikumaanisha ya kwamba wao. . . Wanalitoa nje kwa furaha, badala ya nguvu, imani. Shikilieni hilo hapo na mliamini, Hilo ni Neno la Mungu, dumuni moja kwa moja Nalo.

⁹⁴ Mwangalie Kaini, alikuja na kutoa sadaka, akajenga madhabahu, alikuwa mfuasi wa kanisa, alikuwa mfuasi wa dhehebu, alipiga magoti madhabahuni na kuomba, akamwabudu Mungu, akatoa zaka zake. Iwapo hayo tu ndiyo Mungu anayohitaji, Kaini alihesabiwa haki tu kama Habili alivyohesabiwa. Lakini mnaona, siri yote ilikuwa, ilikuwa ni ufunuo.

⁹⁵ Hapo ndipo shida ilipo, watu hawaelewi ya kwamba Kanisa lote la Mungu aliye hai limejengwa juu ya ufunuo wa kiroho wa Kristo. Yesu alisema hivyo katika Mathayo Mtakatifu 16, “Heri wewe, Simoni, mwana wa Yona, mwili na damu havikukufunulia hili, bali Baba Yangu aliye Mbinguni. Na juu- . . . Wewe ni Simoni, juu ya mwamba huu nitalijenga Kanisa Langu.”

⁹⁶ Wakati ufunuo wa kiroho wa Yesu Kristo, na Yeye ni Neno (“Hapo mwanzo alikuwako Neno, naye Neno alikuwako kwa Mungu, naye Neno alikuwa Mungu. Naye Neno alifanyika mwili, akakaa kwetu.”), basi Neno hilo linapoingia ndani yako, “Ni kali kuliko upanga ukatao kuwili, hata huyatambua mawazo na makusudi ya moyo,” hilo hapo Neno likiingia, ufunuo wa kila Neno la Mungu ni kweli, shikilia nafsi yako kwenye sehemu Yake yoyote, ufunuo.

⁹⁷ Loo, napenda mambo haya. Jamani, nafikiri yanaliweka kanisa mahali ambapo m—mngeweza kuwa na ibada ya uponyaji. Mnaona? Mungu alisema hivyo, hilo latosha, ni hilo—ni hilo tu, Mungu alisema hivyo, dumu tu moja kwa moja nalo.

⁹⁸ Sasa, lakini vipi. . . ? Hakukuwako na Biblia katika siku hiyo, kwa hiyo hapana shaka ilifunuliwa kwa Habili, Waebrania 11 ilisema, “Kwa imani Habili alimtolea Mungu dhabihu iliyo bora kuliko ya Kaini,” ikimshuhudia kwamba alikuwa mwenye haki.

⁹⁹ Sasa, Kaini alisema, “Nadhani mama yangu alikula matofaa, ndipo ikambidi kuvaa nguo.”

¹⁰⁰ Lakini Habili alijua ya kwamba ilikuwa ni damu, uhai, kuna jambo baya lilitukia. Naye akatoa damu ya mwana-kondoo. Ninaweza kumwona akija na maskini mwana-kondoo huyu.

¹⁰¹ Loo, madhabahu ya Shetani ilikuwa nzuri sana kuliko ya Habili, alikuwa na matunda na maua, na yote ni mazuri.

¹⁰² Lakini hilo—hilo ndilo—hilo ndilo ninalojaribu kuliambia Kanisa: Dada, si lazima ujipake rangi ya makucha, na kujirembesha sana, uvae nguo kama huyo mama mwingine upate kujipatanisha na Mungu. Si lazima uwe na kanisa ambalo lina mabENCHI ya dola elfu moja ndani yake, na kinanda cha bomba kilichogharimu dola milioni kadhaa, na madoido haya yote, hivyo vinatoka kuzimu. Hiyo ni kweli, ninaweza kulithibitisha kwa Biblia. Hiyo ni kweli.

Kaini aliwazia mambo haya, “Nitatoa vitu hivi.”

¹⁰³ Lakini ninawazia matoleo ya Habili hayakuwa mazuri sana, labda hakukuwako na kamba yoyote ya katani siku hizo, kwa hiyo hapana shaka alikuwa amefunga shingo ya maskini mwana-kondoo huyo kwa kamba ya mzabibu, akampeleka huko juu, na kumlaza juu ya mwamba. Hakuwa na mkuki wala kisu wakati huo, kwa hiyo hapana shaka alichukua ki—kipande cha mwamba, akakivuta maskini kichwa chake nyuma, akaanza kuikata maskini shingo yake.

¹⁰⁴ Na alipoanza kulia, kurusha mateke, huku damu ikimwagika mwilini mwake, akitokwa na damu, akilia, akifa juu ya mwamba, iliwakilisha nini? Miaka elfu nne baadaye, Mwana-Kondoo wa Mungu alikatwakatwa hata akafa juu ya ule Mwamba wa Miaka, akitokwa na damu, akilia, akinena kwa lugha alipokuwa akifa pale Kalvari.

Loo, ewe Mwana-kondoo mpendwa anayekufa,
 Damu Yako ya thamani
 Kamwe haitapoteza nguvu zake,
 Mpaka Kanisa lote la Mungu lililokombolewa
 Litakapookolewa lisitende dhambi tena.

¹⁰⁵ Mipango yetu ya elimu, mipango ya kimadhehebu haitamaanisha *hilo*, itahitaji Damu ya Yesu Kristo, wala hakuna kitu kingine cha kufanya hivyo. [Ndugu Branham alidata vidole vyake—Mh.] Naam.

¹⁰⁶ Angalieni moshi ukipanda kutoka hapo. Basi kumbukeni, hili hapa, mwaminio: Habili alikufa juu ya mwamba ule ule pamoja na mwana-kondoo wake. Kila mwaminio hana budi kufanya jambo lile lile, kufa juu ya mwamba pamoja na Mwana-kondoo wako.

¹⁰⁷ Mwana-kondoo hana ila kitu kimoja, na hicho ni sufu, naye hana budi kupoteza yote aliyo nayo, haanzishi ubishi juu yake. Hebu mchukue maskini jamaa huyo na kumtupa kule juu, ni kama ilivyosemwa, mwana-kondoo alivyo kimya mbele yao wamkatao manyoya. Anakatwa manyoya, haleti ubishi juu yake. Kitu pekee alichu nacho, anakipoteza, bila fujo.

¹⁰⁸ Nasi tunasema ati sisi ni Wakristo. Mtu fulani aliniandikia barua ndogo hivi majuzi, na, muhtasari mdogo, na kuuweka ndani, nami nikaupata kule chini, kasema, “Nina haki, mimi ni raia wa Marekani, mimi huvaa nguo za aina yoyote ninazotaka.”

¹⁰⁹ Endelea moja kwa moja, ni sawa, hiyo inaonyesha wewe ni mbuzi. Hiyo ni kweli. Wewe endelea tu na uzivae ukitaka. Lakini kumbuka, kama wewe ni mwana-kondoo, una haki kwake, bali unapoteza haki zako kwa ajili ya Kristo.

¹¹⁰ Nina haki ya kulewa usiku wa leo, pia, mimi ni raia wa Marekani; nina haki ya kuvuta sigara, mimi ni raia wa Marekani, unayo, pia, lakini tunapoteza haki zetu, kunyolewa vitu hivyo. Tendeni kama waungwana, kama mama wa heshima, vaeni hivyo, na mtende hivyo, na mwishi hivyo, potezeni haki zenu.

¹¹¹ Angalieni moshi ukipanda juu kutoka madhabahuni, ukipanda moja kwa moja na kutulia pale Kalvari. Kama vile Kaini alivyomwua Habili madhabahuni, Yuda alimwua Yesu madhabahuni. Kweli.

¹¹² Angalieni, tena, mnaona tu misalaba mitatu, sivyo? Kulikuwa na minne, misalaba minne. Kulikuwako na Yesu katikati, mwizi upande mmoja, na mwizi hapo upande mwingine, naye Yuda akajinyonga juu ya mkuyu. Naye Yesu alikuwa ametundikwa juu ya mti, pia, "Amelaaniwa yeye aangikwaye juu ya mti," Naye alifanywa laana kwa ajili yetu. Yuda alikuwa kwenye msalaba kadiri tu Yeye alivyokuwa, maana alikuwa juu ya mti, Yesu juu ya mti kama vile Yuda alivyokuwa, "Amelaaniwa yule aangikwaye juu ya mti."

¹¹³ Angalieni hapa, huyo hapo Mwana wa Mungu, Mungu aliyedhihirishwa, akashuka kutoka Mbinguni, akirudi Mbinguni, akimchukua mwenye dhambi aliyetubu pamoja Naye; na hapo alikuwako Yuda, mwana wa upotevu, aliyetoka kuzimu, akirudi kuzimu, akichukua pamoja naye mwenye dhambi asiyetubu, akirudi tena. Loo, inapendeza!

¹¹⁴ Kama vile Mungu alivyoufungua ubavu wa Adamu katika bustani, na kutoa sehemu ya kufanyia bibi-arusi, Mungu alifungua ubavu wa Yesu pale Kalvari, na kumtoa Bibi-arusi, kutoka ubavuni Mwake. Loo, inapendeza! Pale msalabani, jinsi ilivyo, na jinsi hizo roho mbili, jinsi zilivyokuja kupitia kwa Kaini, Habili, kunguru, hua.

¹¹⁵ Basi angalieni, tunafikiri tena, Kaini, wakati alipoenda kwenye nchi ya Nodi, alijipatia mke. Nasi tunaona ya kwamba mke huyo... Nimeandika Maandiko hapo chini, sitayaandea hayo wakati huu.

¹¹⁶ Waangalieni Israeli, Israeli walipoondoka huko, kama mizabibu miwili, tunaiona ipipanda juu, daima imekuwa hivyo, angalieni, hawa hapa Israeli wanakuja wakienda zao kwenye nchi ya ahadi, kama Kanisa lilivyo siku hizi. Walikutana na nini? Walikutana na Moabu. Naye akatuma watu kwa ndugu yake, na kusema, "Tunaweza kuvukia nchini mwenu? Kama ng'ombe wetu wakila nyasi yoyote, tutailipia, kama wakinywa maji yoyote, tutayalipia." Naye akakataa kuwapisha.

¹¹⁷ Sasa, angalieni hapa, hao hapo Israeli, kundi dogo la wasio na mipaka ya kimadhehebu, wakipitia nchini, hawana mahali pa kutulia, bali wakienda zao nyumbani. . . Moabu walikaa pamoja na watu mashuhuri, waliohesabiwa miongoni mwa mataifa ya ulimwengu.

¹¹⁸ Angalieni kilichotukia, Israeli walikuwa na ule mkondo wa kweli wa damu. Kumbukeni jinsi Balaamu alivyojaribu kuwaoza namna hiyo, ndipo ikambidi kuwafukuza, wanawake na kadhalika. Mafundisho ya Balaamu, fundisho la Balaamu.

¹¹⁹ Angalieni, huyo hapo Moabu, walimwamini Mungu yeye yule ambaye Israeli walimwamini. Kwa kuwa ilikuwa ni nini? Mke mwingine haramu, mwovu, mtoto wa Lutu kwa binti yake. Ni kama tu vile makanisa yasiyozaliwa siku hizi, kanisa la kawaida ni kanisa la ulimwengu, likifanya uasherati wa kiroho na ulimwengu, wala hawaishi waaminifu kwa Mungu, mfano mzuri sana.

Angalieni, tuginena kimsingi. . . Sasa, ndugu wa kimsingi, mimi si. . . Sitaki kukufinya kwa nguvu sana, bali nataka ulihisi.

¹²⁰ Angalieni, huyu hapa a—askofu anashuka, Balaamu, naye akapanda kule, ndipo mfalme akasema, “Shuka uje ukawalaani watu hawa.” Kasema, “Siwataki hapa, hawawezi kufanyia moja ya hizo ibada za uponyaji hapa. Mbona, sikuzote wanazungumza kuhusu uponyaji, nao walisema wana nyoka wa shaba kule chini ambaye wote wanamwangalia na kupata afya. Kisha wanasema wanakula mana kutoka Mbinguni, sikuona yoyote ya hiyo. Na, loo, ni lundo la upuuzi!” Kisha kasema, “Ninataka ushuke uje ukawalaani. Hatutaki chochote cha upuuzi huo kichanganyikane na madhehebu yetu hapa, kwa hiyo wazuie wasiingie hapa.”

¹²¹ Angalieni, yeye alikuwa wa kimsingi tu kama Israeli walivyokuwa, alijenga madhabahu saba, dhabihu saba, kondoo dume saba, hasa kabisa vile walivyokuwa wakifanya huko chini katika kambi ya Israeli, mnaona, dhabihu zile zile. Lakini kile Balaamu alichokosa kuona ni ule Mwamba uliopigwa, yule nyoka wa shaba, makelele ya hiyo kambi, ya Mfalme, alikosa kuona hiyo Nguzo ya Moto ikiwatangulia.

Hivyo ndivyo ilivyo siku hizi, wanasema, “Ninyi ni wa hao Wapentekoste, wao ni kundi la watakatifu wanaojibingirisha.”

¹²² Walikuwa hivyo, lakini hawako hivyo tena. Lakini kwa hiyo, hao—hao ni wao, bali wanashindwa kuona hiyo Nguzo ya Moto. Sasa, kusudi waweze kuhakikisha wataiona, tuna picha Yake, iliyothibitishwa kisayansi. Amina. Naam. Wanashindwa kuona ile Nguzo ya Moto, makelele kambini, kwamba kuna Mfalme miongoni mwetu, amina, Mfalme Yesu. Wanashindwa kuuona. Alishindwa kuona upatanisho huo wa damu.

Wanasema, “Namjua mwanamume Mpentekoste aliyetoroka na mke wa mtu mwingine.”

¹²³ Najua Wabaptisti, na Wapresbiteri wamefanya vivyo hivyo, Wakatoliki, na kadhalika. Hiyo ni kweli. Kwa hiyo sheria ni msumeno, yakata mbele na nyuma; nyungu haiwezi kuita birika kwamba ni nyeusi. Sisi sote ni wanadamu, nasi tuko chini ya mambo hayo yote miongoni mwa watu we—wetu, bali Mungu hushughulika nasi kama watu binafsi, hata tuwe nani. Kwa hiyo baraka za Kipentekoste ni za kweli.

¹²⁴ Angalieni, Israeli na Moabu, sasa ni sawa, tunaona ya kwamba kanisa linachukua ninii, linatoka na kuchukua dhehebu, wanaingiza chochote wanachotaka, wao wanasema tu, “Vema sasa, kama utakuja na kubatizwa kanisani mwetu, na kusimama na kusema unamwamini Yesu Mwana wa Mungu, basi tuta—tutakubatizia kanisani, na kuandika jina lako kwenye kitabu.”

¹²⁵ Sasa, mnajua ibilisi anaamini pia? Hakika, anaamini. Niliwaelezea hivi majuzi usiku, ninyi... Kama vile kujaribu kumzamisha maskini kasa huyu, haikumfanyia chochote, haikumsaidia hata kidogo, ilihitaji moto kumfanya asogee. Na kwa hiyo, huo ndio unaohitajika kwa Kanisa siku hizi, ni Moto kidogo wa Roho Mtakatifu kulifanya lisonge.

¹²⁶ Lakini, kumbukeni, Roho Mtakatifu hatamchukua mtu huyo mchafu amwingize ndani Yake, Mwili wa Kristo. Hiyo inaonyesha ya kwamba Mwili wa Kristo si dhehebu, kwa kuwa ni Mwili wa kisiri wa Kristo, na kwa Roho mmoja sote tumbatizwa ndani Yake. Nafikiri tunaweza kuwachukua wanawake, wanaume, na kuwapeleka majini kuwabatiza, na tunaona kama kweli wao si Wakristo moyoni mwao, hatupaswi kamwe kuwabatiza.

¹²⁷ Nilikuwa nikienda wakati fulani uliopita pamoja na mwanamke mtoni, kundi lao, mwanamke mmoja alitoka akaenda kule; alitoka kwenye gari lake na akavuka, akitengeneza nywele zake, akasema, “Nenda, ukanishushe kule ukanitumbukize, Ndugu Branham?”

Nikasema, “Si wewe, hustahili kuingia mle.” Hiyo ni kweli.

¹²⁸ Walikuwa wakienda kuimba kanisani, ndipo msichana fulani, ha—hakuwa na pesa za kutosha ku—ku—kutengeneza nywele zake kwa mtindo aliotaka kutengeneza apate kupanda jukwaani kuimba, huku maskini mama yake amefua kwenye ubao apate kugharamia mtindo huo wa nywele kwa ajili yake. Hilipopata hiyo habari, nisingemwacha aimbe, nikasema, “Hufai kuimba huko juu.” Hapo panapaswa kudumishwa safi.

¹²⁹ Hiyo ndiyo shida ya makanisa siku hizi, upotovu na kadhalika, moja kwa moja kutoka mimbarani hata kwenye orofa ya chini. Hiyo ni kweli. Yasafisheni! Hiyo ni kweli. Tunahitaji kile kisugulio cha mtindo wa kale tena kanisani.

¹³⁰ Kama vile maskini yule mtu mweusi alivyokuwa akiwekwa wakfu siku moja, nao wazee waliosimama karibu wakasema,

“Bwana, mfunge kwa magunia ya turubai na ummwagilie mafuta ya taa kisha umwashe moto kwa ajili ya Injili.” Hilo ndilo tunalohitaji siku hizi, ashike Moto, umwachilie basi, na umwache atimue mbio.

¹³¹ Tulikuwa tukiwatia ndama chapa. Tungemchukua ndama, najua mmewafunga kamba na kuwafungia wengi, nadhani, tulikuwa tukiwapiga chapa, mtu fulani akaniambia, “Hivi huoni aibu kubeba chuma hicho cha moto, na kukichomelea ubavuni mwake?”

¹³² “La.” Nilikichomelea ubavuni mwake, alikuwa na kifafa cha kurusha mateke, kweli. Alikoroma na kunguruma, alipomwachilia alishikwa na mtukutiko, alikimbia kwelikweli. Lakini tulijua alikuwa wa nani tangu hapo na kuendelea, hiyo ni kweli, almuradi alikuwa hai. Nami nakwambia, ndugu, inahitaji neema nyingi sana kuja madhabahuni na kukaa hapo mpaka Roho Mtakatifu atakapochoma Muhuri ndani yako. Unaweza kupiga mayowe, na kulia, na kutenda kiajabu, bali unajua mahali ulipo tangu wakati huo na kuendelea, hiyo ni kweli, kwa kuwa umetiwa muhuri katika Ufalme wa Mungu na Roho Mtakatifu, Huyo ndiye Muhuri.

¹³³ Kumbukeni, Roho Mtakatifu alikuja kuwatia muhuri wale ambao Mungu alitangulia kuwajua. Hiyo ni kweli. Sawa. Yeye hakushuka tu, Yesu, aseme, “Nitakufa, labda mtu fulani atanihurumia na kuniangalia Mimi, na kusema, ‘Vema, nadhani.’ Labda kama watafikiri niliteseka sana hata itawahuzunisha sana nao watakuja.” La, la. Hutakuja kwa vyovyote vile. Huwezi kumwambia nguruwe amekosea kwa kula kwenye lundo la samadi, yeye atakwambia tu upesi sana, kama angeweza kuzungumza, “Nashika langu, wewe shika lako.” Mnaona?

¹³⁴ Inahitaji wongofu, Mungu hana budi kufanya hivyo, hakuna mtu ajaye kwa Yesu asipovutwa na Mungu kwanza. Inahitaji kazi ya Roho Mtakatifu hata kuugeuza moyo wako, inahitaji Mungu. Mtu fulani alisema, “Nilimtafuta Mungu na kumtafuta Mungu.” La, la, la, Mungu alikutafuta, si wewe kumtafuta Mungu; Mungu hukutafuta.

¹³⁵ Vema, Roho Mtakatifu hachukui tu mke wa aina yoyote, hamchukui mtu anayevuta sigara, na mtu anayekunywa pombe, na mtu anayeishi maisha machafu, na mtu anayeendelea na kila namna ya mambo ya ulimwengu, maana Yeye alisema, “Ukiipenda dunia, mambo ya dunia, kumpenda Mungu hata hakumo ndani yako.”

¹³⁶ Lakini Roho Mtakatifu alikuja kumtia muhuri Mke wa Yesu Kristo awe katika huo Mwili, ambaye alitangulia kumjua kabla ya kuwekwa misingi ya ulimwengu, wakati Yeye, kwa kuwa Mungu katika kujua tangu zamani, angeweza kuona ni nani angempokea na ni nani asingempokea, kwa hiyo Roho Mtakatifu alikuja kumchukua Bibi-arusi *huyo*, huyo Ndiye anayemchukua.

Lakini kanisa linasema, “Loo . . .”

¹³⁷ Nilikuwa nikiimba wimbo mdogo, natumaini sisikiki wa kukufuru, tulikuwa na wimbo mdogo tuliokuwa tukiimba, “Njoni mle,’ Bwana anaita,” tulikuwa na wimbo mdogo nasi tukaufanya tofauti kidogo. Samahani nikiwakwaza kwa njia yoyote. Kasema:

“Njoni mkaj’unge,” mchungaji anaita, “Njoni mkaj’unge;”

Mnaweza kufanya karamu zenu za aiskrimu wakati wote;

Mfanye mizaha michafu, mcheue, na kupuliza moshi,

Loo, mchungaji analiita kusanyiko, “Njoni mkaj’unge.” (Badala ya “Njoni Mle.”)

¹³⁸ Ni tofauti jinsi gani! Kumchukua mtu, maadamu ana pesa kidogo na anaweza kulipa, kumweka kwenye halmashauri ya mashemasi, ana wake wawili au watatu, wanamweka hapo, kwa vyovyote vile, kwa sababu wao ni watu wenye ushawishi mjini. Sijali kama mji unawachukia, ninawataka walio na ushawishi Mbinguni, ambako Roho Mtakatifu, ambako wanaweza kuwa na ushawishi fulani miongoni mwa watu. Lakini ni, “Njoni tu mkaj’unge.” Kila kitu . . .

Nilimwuliza msichana fulani siku moja, “Je, wewe ni Mkristo?”

¹³⁹ Naye akasema, “Nataka ufahamu mimi ni Mmarekani.” Kana kwamba hilo lilikuwa na uhusiano wowote nalo, alikuwa huko Uswisi, kana kwamba hilo lilikuwa na uhusiano wowote nalo.

¹⁴⁰ Ndugu Bosworth alisema alimwuliza mwanamke mmoja wakati mmoja, akasema, “Nataka ufahamu mimi huwasha mshumaa kila usiku.” Sasa, kana kwamba hilo lina uhusiano wowote na Ukristo, kuwasha mshumaa kila usiku. Huna budi kuzaliwa katika *huu*, kuwa Ufalme wa Mungu.

¹⁴¹ Sasa, tunaona roho hizo, angalieni, yapata tu wakati ambapo Yesu alijitokeza jukwaani, Yuda akajitokeza jukwaani; yapata tu wakati Yesu alipoondoka jukwaani, siku ile ile, Yesu na Yuda wote wawili wakaondoka jukwaani. Yapata tu wakati Roho Mtakatifu alipojitokeza jukwaani, ilikuwaje? Mpinga Kristo akajitokeza jukwaani. Kwa maana Yohana anasema hivyo, kasema, “Watoto wadogo msidanganyike nalo,” kasema, “mpinga-Kristo tayari anatenda kazi ulimwenguni.” Mnaona? Haji katika siku hizi za mwisho, tayari yupo, basi, daima amekuwako.

¹⁴² Na sasa, angalieni, yapata wakati mpinga-Kristo anajiinua sasa na kuyachukua makanisa yote, hata Wapentekoste wetu, kwenye hiki chumba kikubwa cha maiti hapa juu, mwajua, makanisa ya UN, mnaelewa ninapomaanisha . . . Ninasikia

baadhi ya madhehebu yetu ya Kipentekoste yanaingia humo. *Hm-Hmm!* Nini...? Jinsi mnavyoweza kwenda mbali na Roho wa Mungu mnapoanza kutangatanga! Mnaondoka upesi kwenye barabara hiyo nyembamba, na mnaendelea tu kuteleza. Hiyo ni kweli. Huna budi kurudi mahali ulipoachia. Hiyo ni kweli.

¹⁴³ Mwungano wa makanisa, ambao utaunda sanamu ya mnyama, nasi sote tunajua hilo. Mnaona, huo hapo, wote ukifanya kazi sasa hivi kuyaleta makanisa yote pamoja, kujiunganisha pamoja wapate kupigana na ukomunisti. Msijali kuhusu ukomunisti, huo hautakuwa ndio kitu cha kupiga vita.

¹⁴⁴ Kuna mapazia matatu, nasema hili katika Jina la Bwana, kamwe msisahau hilo: Kuna pazia la chuma, pazia la mianzi, na pazia la zambarau. Angalieni hilo pazia la zambarau, likazieni macho hilo.

¹⁴⁵ Loo, jamani, jinsi tunavyoona sasa mpinga-Kristo akianza kujifunua, akikita mizizi katika taifa. Hata limemchagua mtu wao wenyewe, hayo makanisa mengine yakiungana naye, yakifanya kiongozi mmoja mkubwa mno, wa kikanisa. Maaskofu wote wa Kianglikana ninii... wanaenda sasa huko Po-... huko Rumi kushauriana na Papa, mara ya kwanza kwa mamia ya miaka. Loo, yote yanachukua uongozi. Na sisi Waprotestanti tunaketi kitako, mwajua, na... Vema, haya basi, unaona, endeleeni tu, kwa sababu limepoa.

¹⁴⁶ Hatutalikomesha, halitakoma, litazidi kuwa baya zaidi. Ni... Biblia ilisema hivyo, ya kwamba kanisa la Kipentekoste katika siku za mwisho, tunajua ni Wakati wa Kanisa la Laodikia ndio ambao unakuwa vuguvugu, ndipo Mungu analitema kutoka katika kinywa Chake, linamchefua tumboni, hawezi kulivumilia, jinsi lilivyo.

¹⁴⁷ Sasa, hebu tuendeleo sasa na tuchukue baadhi ya mihuri hii, na tuifanyie kazi kwa dakika chache zijazo. Twendeni mle sasa, kama mnaandika Maandiko yenu, hebu twendeni katika Ezekieli mlango wa 9. Nasi tunaona ya kwamba huyo nabii alitangulia kuona kuja mara ya kwanza kwa kanisa. Sasa, tunaona ya kwamba aliona, akamwita nabii, naye akaangalia juu kwenye malango ya juu na kusema, "Umewahi kuona kitu kama hiki?" Ndipo wakatokea watu wanne kwenye lango la juu wakiwa na silaha za kufisha mkononi mwao. [Sehemu tupu kwenye kanda—Mh.] ...someni Ezekieli mlango wa 9. Sasa kumbukeni, kuchinja huko kulikusudiwa Yerusalemu pekee, "Piteni katikati ya mji."

¹⁴⁸ Lakini kabla hawajapitia katikati ya mji, walikuta jambo lingine likitukia, alikuja Mtu akiwa na, amevaa mavazi meupe, ana kidau cha wino ubavuni Mwake, kidau cha wino cha mwandishi, Naye akasema, "Wazuieni watu hawa wengine, wasije wakaingia mjini, mpaka kwanza yule Mtu aliyevaa mavazi meupe, mwenye kidau cha wino cha mwandishi, apite

katikati ya mji wa Yerusalemu na kutia muhuri, ama alama, wale wanaougua na kulia kwa ajili ya machukizo yanayofanyika mjini.”

¹⁴⁹ Sasa, Huyu mwenye kidau cha wino ubavuni Mwake, alikuwa ni Roho Mtakatifu. Sasa angalieni, baada ya Yeye kupita, ndipo akawaachilia watu hawa wenye silaha za kufisha, Yeye akasema, “Waangamizeni wote, vijana, wazee, wasichana, watoto wadogo, msiachilie chochote; lakini msimkaribie yeyote wa hao walio na muhuri huo juu yao.” Angalieni hilo.

¹⁵⁰ Sasa, hilo lilitukia lini? Hilo lilikuwa ni kanisa la mwanzoni la Kipentekoste, wakati Roho Mtakatifu alipopita na kulitia kanisa alama. Sasa angalieni jinsi ambavyo historia, kama uliwahi kuchukua vitabu vya Josephus, wakati alipoandika juu ya vile vita vikuu yapata mwaka wa 96. Wakati watu wote... Wakati Roho Mtakatifu... Wakati Yesu alipokuja, akafanya ishara za Masihi, akathibitisha ya kwamba Yeye alikuwa ni Masihi, baada ya kuondoka, Yeye alijiamisha Mwenyewe akaingia Utukufuni, akamtuma Roho Mtakatifu tena, na kuwatia mafuta mitume, wakaenda kote wakifanya ishara zile zile alizofanya Yeye.

¹⁵¹ Walikuwa na nguvu za Bwana. Walinena kwa lugha, wakapaza sauti, kulikuwa na Upepo Mkali Unaoenda kasi uliowajaza, nao wakaenda kote kwa bidii sana hata wakaiteketeza miji kwa Roho Mtakatifu. Nao walifanya nini? Waliwadhihaki, wakawacheka. Hiyo ni kweli. Yesu alisema, “Mkinena dhidi Yangu, nitawasamehe. Lakini Roho Mtakatifu atakapokuja, neno moja dhidi Yake halitasamehewa kamwe.” Nao walitia muhuri kikomo chao cha Milele walipowadhihaki watu waliojazwa na Roho Mtakatifu.

¹⁵² Yesu aliwaambia, kasema, “Sasa, wakati utakuja...” Sasa, inakubidi kuona walimu wengi sana pale wa—walimwuliza Yesu maswali matatu tofauti katika Mathayo 24; akajibu kila moja. Hiyo ndiyo sababu mnaiondoka Adventista ya Sabato na hilo, “Ombeni ili kukimbia kwenu kusiwe katika Sabato, siku ya Sabato au wakati wa baridi kali.” Walimwuliza, “Mambo haya yatakuwa lini? Ishara ya kuja itakuwa ni nini? Mwisho wa ulimwengu?” Na yote, maswali matatu tofauti walimwuliza. Naye akalielezea, kama tu walivyomwuliza pale. Nalo lilitukia, historia inaonyesha ni kweli.

¹⁵³ Angefanya nini...? Ingeleta tofauti gani kama kukimbia kwako sasa, kikimbia kutoka mjini, kungekuwa katika siku ya Sabato? Wakati huo, ma—malango ya mji yalifungwa siku ya Sabato. Ingeleta tofauti gani? Ilionyesha haikuwa ya ulimwengu mzima, kwa kuwa mahali pamoja pangekuwa ni wakati wa kiangazi na majira ya baridi kali mahali pengine. “Ombeni ili kukimbia kwenu kusiwe wakati wa baridi kali, wala siku ya Sabato.” Kwa sababu, katika siku hiyo... Yeye... Walionywa,

kasema, “Hao walio Yerusalemu na wakimbilie Uyahudi.” Uyahudi ulikuwa umefunikwa na theluji wakati wa baridi kali. “Ombeni ili kukimbia kwenu kusiwe wakati wa baridi kali, wala siku ya Sabato.”

¹⁵⁴ Lakini wakati Tito alipokuja, nao wakaona...Yesu aliwaambia, “Mtakapona Yerusalemu imezungukwa na majeshi, ndipo yeye aliye kondeni, asirudi kuchukua koti lake, bali akimbilie vilima vya Yuda kwa nguvu uwezavyo kwenda. Ondokeni humo! Kwa sababu watamkufuru Roho Mtakatifu, na kama wakimkufuru Roho Mtakatifu, wanachukua alama ya mnyama, wala hakuna kitu kilichosalia ila uharibifu.”

¹⁵⁵ Hao Wayahudi, walipoona maafa yakija, walisema, “Sasa tutakusanyika mjini, katika nyumba ya Bwana na kuomba.” Hilo si linasikika la kidini sana, tamu sana? Loo, Shetani anaweza kulifanya lionekane halisi sana. Hakika.

¹⁵⁶ Lakini kumbukeni, Josephus alisema ya kwamba wale watu waliokuwa wala watu, kasema, “Kuna kundi lililomfuata Yesu wa Nazareti aliyeenda huku na huko akiwaponya wagonjwa,” kasema, “Pilato alimwua, nao wakauiba mwili Wake, na kuuweka huko nje mahali fulani, na kuukatakata na kuula.” Walikuwa ni wala watu.

¹⁵⁷ Walichokuwa wakifanya, walikuwa wakila ushirika, mwili wa Bwana. Mnaona? Naye akasema, “Hakuna hata mmoja wao aliyepotea, kwa sababu waliondoka kwenda Uyahudi, kama tu vile Maandiko yalivyowaambia wafanye, kama vile Yesu alivyokuwa amewaambia wafanye.”

¹⁵⁸ Lakini hao Wayahudi, wote waliingia Yerusalemu, nao wakasema, “Sasa, tutakusanyika katika nyumba ya Bwana, na Yehova mkuu, Yeye ambaye amekuwa pamoja nasi daima, atashuka chini, Naye atayafukuza majeshi ya Tito, hivyo ndivyo atakavyofanya.”

¹⁵⁹ Lakini walifanya nini? Walikuwa wametenda dhambi dhidi ya Roho Mtakatifu, wangedhihaki nguvu za Roho Mtakatifu zikitenda kazi. Walimwita Yesu Kristo, aliyekuwa akitenda na kuwaonyesha ya kwamba Yeye alikuwa ndiye Masihi wao, walimwita Beelzebuli, wakamwita ibilisi, wakamwambia ilikuwa namna fulani ya telepathia, kasema Yeye alikuwa ni ibilisi, kazi alizokuwa akifanya, zilikuwa ni kazi za ibilisi. Liliwarudia.

¹⁶⁰ Sasa, ndugu, ngojeni tu, hatutapata wakati usiku wa leo, lakini kesho usiku ninataka kuwachukua na kuwaonyesha ya kwamba Marekani imefanya jambo lile lile, hasa. Nitawathibitishia kwa Maandiko, kesho usiku, Bwana akipenda, jinsi Marekani imefanya jambo lile lile, hasa, katika miaka hii arobaini iliyopita. Wamewadhihaki na kuwaita watakatifu wanaojibingirisha, walokole wa Kipentekoste, na kila kitu ulimwenguni, naye Mungu akifanya kazi pamoja nao kwa

ishara na maajabu, nayo makanisa makubwa yameketi tu namna *hii*, na kufanya mzaha. Na sasa katika siku za mwisho, ni jambo gani lililotukia? Hebu niwaletee Maandiko. Mko tayari?

¹⁶¹ Ninatofautiana na Ndugu yangu mpendwa David duPlessis, akienda kule pamoja na Dk. McKee na makanisa haya yote makubwa. Na sasa watafanya nini... [Sehemu tupu kwenye kanda—Mh.]... sasa. Loo, Wapresbiteri wanasema, “Tunahitaji wenye kunena kwa lugha. Tunawataka wapate ubatizo wa Roho Mtakatifu. Tunahitaji waponyaji wa Kiungu,” na yote namna hiyo.

¹⁶² Kwa nini hawakuukubali miaka arobaini iliyopita wakati ulipotokea, badala ya kuudhihaki? Kamwe hawataupokea. Wamekufa, wao ni madhehebu, na kila dhehebu limekufa. Kweli kabisa. Kamwe halitainuka tena. Hakuna dhehebu litakaloinuka kamwe. Waassemblies, mmekuwa na siku yenu; wa Umoja, mlikuwa na siku yenu; Foursquare, mlikuwa na siku yenu, wakati wa Bibi McPherson; Assemblies wa kizamani walikuwa na siku yao.

¹⁶³ Vema, mmefanya nini? Mmejiundia dhehebu na kujitenga. Kamwe hamtaingiza dhehebu, kwa sababu kwanza kabisa lilikuwa ni utaratibu wa Katoliki ambao Mungu aliuhukumu hapo mwanzoni, kamwe halitaingia, hakuna Mbaptisti, Mpresbiteri, wala chochote kile. Lakini Mungu atauvuta moyo wenye njaa kutoka kwa kila dhehebu anaoweza, kwa kuwa huo ni Mwili Wake ambao atauingiza, wale waliotiwa muhuri na Roho Mtakatifu.

¹⁶⁴ Tayari wamechukua alama ya mnyama. Liangalieni sasa, kanisa la Kipentekoste tayari limeonyesha jinsi lilivyo hasa, sasa limetapikwa. Yesu akiwa nje, akibisha, akijaribu kuingia ndani. [Ndugu Branham aligongagonga mimbarani—Mh.] Anabisha nini? Ubishaji wenyewe wa Kimasihi, na kadhalika, nao wangali walimfukuza. Bila shaka, wanafanya hivyo.

¹⁶⁵ Lakini nini kimetukia? Tunaishi katika siku gani? Loo, ndugu yangu, tunaishi katika siku gani? Sidhani nina kichaa, natumaini sina. Kama nina kichaa, niacheni tu, ninajisikia vizuri zaidi hivi, kuliko nilivyojisia vinginevyo. Lakini sikilizeni, sikilizeni, nawaambia, ndugu yangu na dada, ni ishara ya nini? Ni ishara ya kwamba tuko kwenye wakati wa mwisho. Yesu alisema nini kuhusu mwanamwali aliyelala?

“Loo, ati mnayaita hayo makanisa bikira?”

¹⁶⁶ Kama vile tu Kaini alivyokuwa, kitu kile kile hasa. Wanaabudu, bali yule mwanamwali aliyelala hakuwa na Mafuta katika taa yake. Hiyo ni kweli? Kwa hiyo alipoona kwamba alikuwa amechelewa kuliko alivyodhania, ukomunisti ukimnyemelea, alisema, “Loo, tupeni Mafuta yenu kidogo. Unampataje huyu Roho Mtakatifu?”

“Nendeni mkayanunue kutoka kwake yeye anayeyauza.”

¹⁶⁷ Pia kumbukeni, wakati ule ule ambapo yule mwanamwali aliyelala alienda kununua Mafuta, hapo ndipo Bwana-arusi alipokuja. Utukufu! Hivi hamlioni? Kama Wapresbiteri, na Waepiskopolia, na hao wengine, wamekuja wakimtafuta Roho Mtakatifu, afadhali uitengeneze taa yako. Itengenezwe, itengenezwe, naam, inahitaji kutengenezwa. Enyi Wapentekoste, afadhali mwe mkizitengeneza taa. Amina. Katilieni mbali ulimwengu huu mwingi kutoka kwenu. Tayari mmeota kutu, utambi umechafuka vibaya.

¹⁶⁸ Mnajua, utambi huo ni kitu kikuu. Nilikuwa nikininii... Angalieni, kile utambi halisi wa Mungu ulicho, mwa—mwaminio, ni utambi. Angalieni, yeye ana Moto upande mmoja, *hapa* juu, halafu upande huo mwingine umetumbukizwa katika Mafuta, ukivuta Mafuta na kuwaka Moto. Ni—ni Kanisa la jinsi gani! Ni nguvu za jinsi gani! Ni mahali pa jinsi gani kuwako! Haleluya!

¹⁶⁹ Ikiangaza, Nuru ile ile ya Injili iliyoangaza mashariki, inaangaza magharibi. “Itakuwa Nuru wakati wa jioni.” Inuka, itengeneze taa yako, Pentekoste, ukatilie mbali ulimwengu, ikatilie mbali mitindo ya ulimwengu, yakate na kuondoa mambo ya ulimwengu, kuwa tayari, wakati umewadia.

¹⁷⁰ Mara walipoenda kununua Haya, ilikuwaje? Ni kitu gani kilichotukia? Ndipo Bwana-arusi akaingia.

¹⁷¹ Mnaona, Marekani imemkufuru Roho Mtakatifu. Imemdhihakiki tangu alipotokea jukwaani miaka arobaini ama hamsini iliyopita. Sikuzote imemdhihakiki, hayo makanisa mengine yamedhihakiki, yamejionyesha yenyewe, sasa wanaanza kuinua vichwa vyao, na kusema, “Tungetaka kuwa na Haya kidogo.” Lakini mara tu wanapoanza kwenda kufanya hivyo, ni ishara kwamba tunapaswa kuanza kuitengeneza taa yetu.

¹⁷² Mungu na awainue wahubiri wengine watakaoenda kuzitengeneza taa. Ninawaambia kile tunachohitaji siku hizi ni kitu kitakachoitengeneza taa yetu, ili Moto wa kweli wa Kipentekoste...

¹⁷³ Ukiona taa ya kale imefikia kabisa mahali ambapo kababoni inaingia kwenye utambi wa taa, itaijaza taa yako moshi. Hiyo ndiyo shida yetu, tuna kaboni nyingi kupita kiasi kwenye taa, kaboni nyingi kupita kiasi, Moto hauwezi kuwaka vizuri, hauwezi kupata hewa ya kutosha kutoka chini. Tunachohitaji ni kipindi kizuri cha kupumua, pumzi nzuri, pumzi mpya kutoka Mbinguni ya ubatizo wa Roho Mtakatifu tena, na Roho Mtakatifu akitenda kazi Kanisani huku ishara na maajabu yakifuata, ule Muhuri wa kweli wa Mungu.

¹⁷⁴ Si kusema, “Vema, nitaenda kwenye Assemblies, wasiponitendea mema, nitaenda kwenye Foursquare.” Loo, umejaa kaboni, unatia nuru yako moshi. Tengeneza taa yako! Jiweke tayari, tuko katika wakati wa mwisho.

¹⁷⁵ Lakini wataninii, mtu fulani atalihubiri, mtu fulani atalisema, mahali fulani kutakuwa na baadhi yao watakaolipata. Hiyo ni kweli. Sijui ni wangapi, maana Yeye alisema, “Kama ilivyokuwa katika siku za Nuhu, ndivyo itakavyokuwa katika kuja kwake Mwana wa Adamu, ambapo watu wanane waliokolewa.” Lakini sijui ni wangapi watakaolipata, bali kutakuwa na baadhi yao watakaoitengeneza taa yao, ni hayo tu, kwa maana wakati wa kutengeneza taa unaendelea.

¹⁷⁶ Na wakati nanii—wakati yule mwanamwali aliyelala alipotoka, ambaye tayari alikuwa amepokea alama ya mnyama...

Unasema, “Alama ya mnyama, hiyo?”

¹⁷⁷ Naam, kweli. Vivyo hivyo Kaini alipokea hiyo chapa kisha akaondoka. Ilikuwa ni kitu gani? Wakati kanisa la Kibaptisti, wakati kanisa la Kipentekoste, wakati kanisa la Presbiteri, lilipochukua alama ya mnyama badala ya kumpokea Roho Mtakatifu, walitoka kwa Mungu, na kujiundia dhehebu. Walifanya nini? Walijichukulia mke bandia, mke bandia wa ulimwengu, wakawaingiza Mayezebeli waliojipodaa, na kadhalika, wakiwa na nywele fupi, na kuvaa kaptura, na sketi, na, za mtindo wa Hollywood, nao wahubiri wakaanza kuwaingiza ndani pamoja na mashemasi walio na wake wawili au watatu. Na—na mtu...

Unasema, “Sikuzote unazungumza juu ya wanawake wetu, kuhusu wanawake wetu.”

¹⁷⁸ Vema, enyi wanaume, nitawachambua mara moja basi. Hebu niwaambieni jambo fulani: Mwanamume yeyote ambaye atamwacha mke wake avute sigara na kuvaa kaptura, hata sina heshima kwake kuwa mwanamume, yeye ni dondoadume sana hata hajui yeye ni wa nani, yeye si mwanamume. Hiyo ni kweli. Loo, haleluya! Sawa. Yeye ni kisingizio duni cha mwanamume. Loo, huenda akawa na urefu wa futi sita, awe na uzito wa ratili mia mbili, lakini huyo haonekani kama mwanamume kwangu mimi. Hiyo inaonyesha ni nani bosi nyumbani mwako. Atakanyaga kwa kishindo, “Hebu nikwambie sasa hivi,” nawe ungeinama kana kwamba ulikuwa mtoto mgonjwa wa paka. Kuna nini?

¹⁷⁹ Tunahitaji, tunachohitaji leo hii ni wanaume. Tunahitaji wahubiri wa Injili. Na mhubiri yeyote atakayesimama mimbarani, na kujizuia kusema mambo hayo, nina heshima duni kwake kwamba aliitwa na Mungu. Hiyo ni kweli. Mtu anayeona aibu kusimama mimbarani na kusema kweli ya Mungu, wakati anajua ni utovu wa uadilifu kwa mwanamke kukata nywele zake!

¹⁸⁰ Biblia... Mwanamume ana haki ya kumwacha mkewe na kumpa talaka anapokata nywele zake, Biblia ilisema hivyo. Ni

nani kichwa cha mwanamke? Mumewe. Nayo Biblia ilisema, “Mwanamke akikata nywele zake, yuaaibisha kichwa chake.” Hakuna mwanamke asiye na heshima anayepaswa kuishiwa naye. Amina. Anakatilia mbali utukufu wake. Na vivyo hivyo na kanisa, wakati linapofanya jambo lile lile, linakatilia mbali mkondo wa utukufu wake.

¹⁸¹ Hmm! Ee Mungu, kwa nini ninasema mambo haya? Lakini ni kweli. La, hatu—hatuhitaji wenye kupatana, tunahitaji wanaume na wanawake ambao watatetea haki na uadilifu na kusema kweli, bila kujali ni nini. Amina.

¹⁸² Muhuri wa Mungu, zitengenezeni taa zenu, ndugu yangu. Hebu nuru ya Roho Mtakatifu iwake tena, upya. Giza linaingia. Loo, ni wakati wa kutisha sana! Giza linaingia.

¹⁸³ Hapa wakati fulani uliopita nilishuka, nilikuwa nikitoka Dallas na nilikuwa nikiruka kwa ndege kuelekea Indiana, ndipo dhoruba ikatokea na—nayo hiyo ndege ilibidi ishuke huko Memphis. Na mimi—mimi... Wakaniweka kwenye ile hoteli kubwa, nzuri huko chini, na kuniambia, walinipigia simu baada ya kitambo kidogo, kasema, “Tutakupigia simu asubuhi saa moja. Tutakuwa na, tutatumia usafiri fulani kukuchukua.” Kwa sababu wangeninii. . . Tayari nilikuwa nimelipia safari yangu, na i—iliwabidi wanilipie hiyo hoteli usiku huo.

¹⁸⁴ Kwa hiyo nikaketi na kuwaandikia marafiki zangu barua. Kesho yake asubuhi nikaamka na nilikuwa nikishuka kwenda kuzituma hizo barua, nami nilikuwa nikishuka kwenda barabarani, nikawazia, “Nitaharakisha sasa kwa sababu limozini hiyo itatuchukua wakati fulani.”

Ndipo nikaanza kushuka barabarani, nikitembea upesi sana, mwajua, Roho Mtakatifu akasema, “Simama kimya.”

Nikaangalia kote, huku askari mkubwa wa Kiairishi amesimama pale, akaangalia huku, nami nikawazia, “Hakika, huyo siye aliyesema hivyo.”

Ndipo nikaanza kutembea tena, kasema, “Njoo kando.”

¹⁸⁵ Basi kulikuwako na vigurudumu vya kuvulia samaki na kadhalika pale, nikaenda namna *hii*, nami nikawazia ningejifanya tu kana kwamba ninaangalia hivyo kusudi asishuku jambo fulani. Kwa hiyo nikaenda pale na kuanza kuangalia vigurudumu hivyo, kisha nikasema, “Baba wa Mbinguni, huyo ni Wewe uliyenena?”

Akasema, “Geuka, na uende kaskazini, na uendelee kutembea.”

¹⁸⁶ Nikasema, “Naam, Baba.” Nikaanza tu. Mnaamini watoto wa Mungu wanapaswa kuongozwa na Roho wa Mungu? Kweli mnaamini. Hiyo ndiyo shida yetu, taa zetu zimeingia moshi sana hata hatuwezi kujua lolote tena.

¹⁸⁷ Sisi hapa, nikaanza kutembea, nikatembea, na nikatembea, na nikatembea, ndipo nikawazia, “Vema, jamani!” Nikaangalia, wakati wa ndege kuja, Naye akaendelea tu kusema, “Tembea,” nikaendelea tu kutembea. Nikaenda kule nikafika, upande wa pili, ndipo nikaingia huko, wilaya ya watu weusi kule.

¹⁸⁸ Nami nilikuwa nikishuka chini, vema, ninii, ilikuwa juu sana, jua lilikuwa juu sana, nami nikawazia, “Loo, nimeachwa na ndege yangu, vema, kama Yeye alisema nitembee, nadhani labda Yeye anamaanisha tutaenda nyumbani kwa miguu, kwa hiyo nitaendelea tu kutembea, niache sanduku langu huko nyuma.” Kwa hiyo basi nikaenda—nikaenda... Sanduku langu bado lilikuwa hotelini, nami nilikuwa na barua hizi, nikaendelea kutembea, nikawazia, “Vema, Bwana...”

Kitu fulani tu kikaendelea kusema, “Endelea kutembea, endelea kutembea,” nikaendelea tu kutembea.

¹⁸⁹ Hilo ndilo jambo pekee la kufanya, haidhuru inaonekanaje, endelea tu, kwa vyovyote vile. Kama Mungu alisema ulifanye, endelea tu, kwa vyovyote vile. Hivyo ndivyo unavyofanya. Hiyo ndiyo njia ya kupata afya, unaona, endelea tu kutembea. Unasema, “Jana nisingeweza kutikisa kidole changu ila kiasi *hicho*, leo hii ninaweza kukitikisa kiasi *hicho*, Mungu asifiwe, kesho, nitakitika kiasi *hicho*, na kesho yake kiasi *hicho*, halafu muda si muda, ninaninii...?...” Endelea tu kutembea, hivyo tu, endelea tu kutembea.

¹⁹⁰ Ndipo nikafika kule upande mwingine wa Memphis, na nilipofanya hivyo, mbona, nilikuwa nikishuka kwenye baadhi, wilaya kubwa ya watu weusi kule, maskini vitu kama vibanda, huko nje. Ndipo nikawaza, “Kwani ninafanya nini hapa?” Nikawaza, “Vema, Yeye alisema niendele kutembea. Kama alitaka nigeukie njia nyingine, angeniambia.” Kwa hiyo nikaendelea tu kutembea. Nami nikatembea, nami nilikuwa nikiimba maskini wimbo ule ninyi Wapentekoste huimba, hebu tuone kama ninaweza kupata hiyo sauti:

Walikuwa wamekusanyika katika chumba cha
juu,
Wote wakiomba katika Jina Lake,
Wakabatizwa kwa Roho Mtakatifu,
Ndipo nguvu zikaja kwa ajili ya huduma;
Sasa, yale aliyowafanyia siku hiyo
Atakufanyia vivyo hivyo,
Nina furaha sana kwamba ninaweza kusema
mimi ni mmoja wao.

Mmeusikia, siyyo? Naam, bwana.

Watu hawa huenda wasijifunze kuwa,
Au kujivunia sifa za ulimwengu,
Wote wameipokea Pentekoste yao,
Kwa imani katika Jina la Yesu;

Nao wanatangaza sasa, mbali na kwa upana,
 Nguvu zake zingali ni zile zile,
 Nina furaha sana kwamba ninaweza kusema
 mimi ni mmoja wao.

¹⁹¹ Nilikuwa nikienda kule, nikiuvumisha huo moyoni, nikaangalia, nikamwona maskini mwanamke mweusi ameegemea kwenye la—la—lango, pale namna *hii*, na ilikuwa huko juu kabisa, na loo, ni majira mazuri ya kuchipua, na ya mauanyuki. M—m—mnafikiri maua ya mchungwa yananukia vizuri, ngoja tu mpaka utakaponusa mauanyuki Indiana huko nyuma. Kwa hiyo, na kulikuwa na... Naye alikuwa ameinama huko nje, huku amejifunga shati la mwanamume kichwani mwake, uso mkubwa mno, mnene, mwajua.

¹⁹² Nami nilikuwa nikija, nikawazia... Vema, nilimwona amesimama pale, nikaendelea kutembea namna *hiyo*, basi nilipokaribia, akaanza kucheka, machozi makubwa mno yakaanza kutiririka machoni mwake. Nikasema, “Habari za asubuhi, Shangazi.” Hivyo ndivyo kwa kawaida tungewaita watu weusi huko kusini.

Akasema, “Habari za asubuhi, Kasisi.”

Nikasema, “Kasisi?” Huyu ni mhubiri, mwajua. Nikasema, “Ulijuaje nilikuwa kasisi?”

Akasema, “Nilijua ulikuwa unakuja.”

Nikasema... Nikasimama na kugeuka nyuma, nikawaza, “Baba, huyu ndiye? Unanituma huko kwa mwanamke huyu wa Kinegro?”

Naye alikuwa amesimama pale, nami nikasema, “Ulijuaje mimi ni kasisi?”

Akasema, “Hivi—hivi uliwahi kusoma hadithi ile kuhusu yule mwanamke Mshunami?”

Nikasema, “Loo, naam.”

¹⁹³ Akasema, “*Mimi ni mwanamke wa namna hiyo.*” Kisha akasema, “Sikuwa na watoto wowote, nami nikamwambia *Bwana* kama angenipa mtoto ambaye ninge—ambaye ninge—ningemlea apate ku—kumtumikia Yeye,” kisha kasema, “Ni—nilimpata. Bwana alinipa mtoto,” kisha kasema, “Nilifanya vibarua vya kufua nipate kumlea.”

¹⁹⁴ Kisha kasema, “A—alikuwa mvulana mzuri sana,” lakini kasema, “alipitia barabara mbaya, akaambatana na kundi baya.” Kisha kasema, “Yeye,” naye alikuwa maskini mtakatifu wa Kipentekoste, na kwa hiyo, akasema, yeye, “alichukua njia mbaya,” na kasema, “ana ugonjwa mbaya sana wa zinaa.” Kisha kasema, “Sikujua hilo.” Kisha kasema, “Sasa hawawezi kumfanyia lolote,” kasema, “moyo wake umekwisha kuliwa.” Kasema, “Yeye amelala mle ndani, akifa.”

¹⁹⁵ Kisha kasema, “Jana usiku niliomba usiku kucha.” Kasema, “Amepoteza fahamu kwa siku mbili, Kasisi.” Kisha kasema, “Niliomba usiku kucha, jana usiku.” Nami nikasema, “Bwana, nipe mtoto huyu,” kasema, “Mimi—mimi ni mtumishi wako,” kasema, “yuko wapi yule Elisha,” akasema. Kisha kasema, “Nikaendelea kuomba.”

¹⁹⁶ Kasema, “Leo asubuhi nilishikwa na usingizi huku nimepiga magoti,” naye akasema, “yapata saa nane.” Ndipo akasema, “Niliota kwamba Bwana aliniambia, ‘Njoo hapa, simama kwenye lango hili.’” Ndipo akasema, “Basi kasema, ‘Yeye atashuka kuja mtaani amevaa suti ya hudhurungi, na kofia ndogo, ya hudhurungi.’” Kisha kasema, “Nimekuwa nikingojea hapa tangu kabla ya mapambazuko, ndipo nikakuona ukija,” kasema, “hiyo. . .ni—nilijua.” Loo, hiyo ndiyo Pentekoste, hiyo ndiyo Pentekoste halisi.

Nikamwambia, nikasema, “Jina langu ni Branham, Shangazi. Uliwahi kusikia habari zangu?”

Akasema, “Hapana bwana, Kasisi Branham, sijawahi kusikia habari zako.” Naye akasema, “Samahani, lakini sijawahi kusikia habari zako.” Akasema, “Hivi hutaingia?”

Nami nikasema, “Naam, mama, asante.” Kamwe sikusema neno lingine. Nikawaza, “Hii haina budi kuwa ndiyo.”

¹⁹⁷ Kwa hiyo nilipoingia, walikuwa na plau iliyokuwa imening’inizwa kwa mnyororo langoni kulirudisha pamoja. Nikaingia nyumba ya maskini vyumba viwili, kile tunachoita nyumba ya marisau huko mashariki, chumba kidogo kirefu.

¹⁹⁸ Nami nimekuwa kwenye majumba ya mfalme, nilienda kumwomba Mfalme George wa Uingereza, Nilikuwa pamoja na Gustaf huko Uswidi, na nimekuwa katika majumba mengi ya kifalme, na Mfalme Farouk, na—na mahali pengine pengi, na watawala wakuu na wafalme, baadhi ya walio wakuu sana ulimwengu ulio nao leo, nimekuwa na majaliwa ya kuingia, kuzungumza nao, kuhojiwa, nimekuwa katika nyumba nzuri, lakini sikukaribishwa zaidi, na kujisikia nyumbani zaidi, kuliko nilivyojisikia katika kibanda hicho kidogo cha Mnego, asubuhi hiyo. Nilipoingia mle, hapakuwapo na zulia sakafuni, kitanda kidogo cha bango kimewekwa namna *hiyo*, nao walikuwa na bango kubwa pale mlangoni, lililosema, “Mungu ibariki nyumba yetu.”

Nimekuwa katika nyumba za watu wanaojiita Wakristo, na picha zilizobandikwa na picha chafu, za vitu ukutani.

Nilijisikia nyumbani kabisa.

¹⁹⁹ Nikaangalia pale kitandani, na hapo alilala mvulana mkubwa mno, mwenye sura shupavu, mweusi, nadhani angekuwa na uzito wa ratili mia moja na sabini, naye alishika blanketi mkononi mwake akifanya, “*Uhm! Uhm!*”

Nikasema, “Kuna nini, Ndugu?”

Naye akasema, “Kasisi, hajazungumza kwa siku mbili.”

Naye akaendelea kusema, “Kuna *giza* humu ndani. Kuna *giza*. Sijui ninakoelekea. *Uhum! Uhum!*”

²⁰⁰ Ndipo maskini yule shangazi akanijia, akasema, “Kasisi, anafikiri yuko huko mtoni mahali fulani, bahari, na kuna giza, naye anapiga makasia mashua wala hawezi kuona anakoelekea.” Kisha kasema, “Amekuwa akisema hivyo kwa siku mbili.”

²⁰¹ Nami nikasema, “Loo, hilo ni baya sana.” Nami nikasema, “Vema, Shangazi,” nikasema, “huduma yangu, ndiyo kwanza nitoke Dallas, Texas, mimi huwaombea wagonjwa.” Hakuvutiwa na hilo.

²⁰² Akasema, “Jambo moja tu ninalotaka kusema, Kasisi. Ninakutaka uombe, na kama Mungu wa Mbinguni atanijalia tu kusikia mvulana wangu akisema, ‘Mama, ni sawa, nimeokoka,’” kasema, “nitakuwa tayari kumwacha aende.” Kasema, “Lakini nimefanya kazi kwa bidii sana, na kuomba sana kwa ajili ya mvulana wangu,” kasema, “Ninachukia tu kumwona akifa namna hiyo, na kujua anaondoka wakati amepotea, amerudi nyuma jinsi alivyo.” Kasema, “Laiti ningemsikia akisema, ‘Ni sawa, Mama, niko tayari kwenda!’ Utaomba?”

²⁰³ Nikasema, “Vema, Shangazi.” Ndipo tukapiga magoti sakafuni, nami nikamwona akiwa na hilo, ama, nadhani, shati la mwanawe limefungiwa kichwani mwake, maskini mashavu makubwa manene mno namna hiyo, naye, mwanamke mkubwa mno, akapiga magoti. Nikawaza. . . Nikasema, “Shangazi, wewe tuongoze katika maombi.”

²⁰⁴ Loo, ndugu, kama kamwe nisingalijua alikuwa Mpentekoste basi, ningalijua hilo wakati huo. Nena kuhusu kuomba! Maskini mwanamke huyo aliomba ombi ambalo lingeninii tu, ungeweza tu kuhisi nywele zako nyuma ya shingo yako zikisimama. Aliomba kama, nawaambia, alizungumza Naye kama aliyekuwa amezungumza Naye hapo awali, alijua ni Nani aliyekuwa akizungumza naye. Wakati. . . Loo, ombi kama hilo, aliugusa tu moyo wangu. Basi alipomaliza, akanyosha mkono, akambusu kichwani, akasema, “Mungu ambariki mtoto wa mama.”

²⁰⁵ Nikawaza, “Hilo hapo, hilo hapo.” Mnaona? “Mungu ambariki mtoto wa mama.” Ingawa alileta fedheha juu ya hiyo nyumba, jamaa mkubwa mno, mwenye sura nzuri namna hiyo, haidhuru amefanya nini, yeye angali ni mtoto wa mama, maana upendo huo wa mama ungali unamwendea.

Nikawaza, “Naam, hiyo ni kweli.”

²⁰⁶ Lakini Biblia ilisema, “Je, mama anaweza kumsahau mtoto wake mchanga anayenyonya?” Kasema, “Huenda akafanya hivyo, bali Mimi siwezi kuwasahau, majina yenu yamechorwa katika vitanga vya mkono Wangu.” Ni tofa-. . . ni upendo mkuu

jinsi gani, jinsi Mungu asingetusahau kamwe! Ingawa taa zetu zimejaa moshi, Yeye angali anatupenda. Hebu tutengeneze tu taa yetu dhaifu, ndugu yangu, hebu na tujitokeze. Hebu—hebu na tujitayarishe kumlaki Bwana Yesu, hebu tujisafishe, hebu tujiandae, tuombe, na tuwe sawa.

Hapo, akambusu namna hiyo. Akasema, “Loo, kuna giza, Mama. Loo, kuna giza,” akivuta kifuniko hicho huku na huku.

Nami nikashika miguu yake, miguu yake ilikuwa baridi na inanata, ndipo nikasema, kama tu kwamba alikuwa yuafa, nami nikasema, “Unaweza kunisikia, Ndugu?”

²⁰⁷ Akasema, “Loo, Mama, kuna giza,” akasema. Nami nikajaribu kuzungumza naye, hakujua, alikuwa akitikisa kichwa chake namna *hiyo*, huku vitu vikitoka kinywani mwake. Naye akasema, “Loo, Mama, kuna giza, kuna giza. Sijui mtumbwi wangu unaelekea wapi,” namna hiyo.

Naye mama akaanza kulia, akiyapangusa maskini hayo mashavu makubwa, namna *hiyo*, ndipo akasema, “Unaona ninalomaanisha, Kasisi?”

Nikasema, “Naam, mama.”

Akasema, “Je, utaomba basi, Kasisi?”

Nikasema, “Naam, mama.” Ndipo nikapiga magoti, nikasema, “Piga magoti pamoja nami.”

²⁰⁸ Nami nikaweka mikono yangu juu ya miguu yake, Nikasema, “Baba wa Mbinguni, ni baada ya saa tatu sasa, ndege yangu imeondoka muda mrefu.” Nikasema, “Na—nakuomba uturehemu. Sijui ni kwa nini uliniongoza hapa, hakika hapa ndipo mahali hapo, hapa ndipo, maana nisingekuja huku kama hukuniongoza, na mwanamke huyu aliyesimama hapa, kamwe hukutuongoza bure, Wewe daima hutuonyesha kile Wewe—kile unachofanya Wewe. Kwa hiyo ninaomba, Baba, kama—kama haya ni mapenzi Yako, ya kwamba utamjalia huyu mvulana . . . mjalie huyu mwanamke hiyo haja, na mjalie . . . naomba aoko, ninaomba ya kwamba utauponya mwili wake.”

²⁰⁹ Basi wakati nilipokuwa nikiomba, akasema, “Mama, loo, Mama, nuru inaingia chumbani.” Ee Mungu! “Nuru inaingia chumbani.” Mwajua, katika dakika chache alikuwa ameketi kando ya kitanda akizungumza nasi, akanikumbatia kwa mkono huo mkubwa, mweusi, namna *hiyo*.

²¹⁰ Nikasema, “Sina budi kuondoka.” Ndipo nikaanza kushuka barabarani, nami nikachukua teksu, nikakimbia kule upesi sana na kuchukua sanduku langu, nikasema, “Vema, nitaondoka, nipande ndege usiku wa leo.” Kulikuwa kubaya sana, mara baada ya vita kule, na ni kubaya sana wakati . . . kupata ndege ya kutoka. Na mara tu nilipoingia, wakasema, “Mwito wa mwisho wa ndege namba 172, kuelekea Louisville.” Hiyo ndege

ilikuwa imekaa ardhini wakati huo wote, nikapanda ndege ile ile. Mnaona, Mungu hufanya kila kitu kitende kazi vizuri, sivyo?

Yapata mwaka mmoja baadaye nilikuwa nikitaka kuninii . . . [Ndugu mmoja ananena kwa lugha, mwingine anafasiri—Mh.]

²¹¹ Mungu, Ee Baba, jinsi tunavyokushukuru kwa ajili ya onyo hili kwetu! Bwana, najua si bure. Ee Mungu, jalia watu waone tunajaribu tu kuwafanya watengeneze taa zao, wawe tayari. Saa inakaribia, Bwana, wakati ishara hizi zote, mwanamwali aliyelala sasa akitafuta Mafuta, mambo haya yote, kumsikia Roho Wako akishuka na kuuthibitisha Ujumbe huu, ya kwamba ni kweli!

²¹² Mungu, ninaomba ya kwamba utawabariki hawa watu, jalia waonywe na Mungu usiku wa leo, wala wasione raha hata watakapokuwa wametengeneza taa zao, na—na wakajiandaa kumlaki Bwana—arusi. Tujalie, Baba. Amina.

²¹³ Ni nzuri jinsi gani! Je, mlimwona mtu huyo? Mliona jinsi wao . . . ? Ninyi—ninyi Wapentekoste kwa kuruhusu upambanuzi uwatatanishe? Angalieni jinsi hili lilivyo kubwa kuliko huo. Mnaona? Jinsi ambavyo—ambavyo, mnaona, mvumo wenyewe wa sauti ambayo mtu huyo alikuwa akitoa, mnaona hiyo tafsiri ikija vivyo hivyo, mnaona, kwa njia ile ile? Yapata urefu ule ule, idadi ile ile ya aya, na kila kitu. Ni Roho Mtakatifu. Ninawaambia kweli, ni kweli.

²¹⁴ Loo, ewe rafiki mwenye dhambi, mtafute Bwana sasa, mwite wakati Yeye—wakati Yeye anaweza kusikiwa. Msikieni Yeye, msikieni Yeye ndiyo maombi yangu.

²¹⁵ Ninataka kuwaambia kilichotukia. Mwaka mmoja baadaye nilikuwa nikipita kwa garimoshi, nikija Phoenix. Kama uliwahi kuwa huko Memphis, ukija kutoka mashariki, unatokea namna *hii*. Nikashuka kwenye garimoshi, nikaanza kutembea kupitia pale. Garimoshi, wanakupa yapata . . . wanakutoza senti hamsini kwa sambusa ndogo, nayo ni nyembamba sana. Basi nikangojea mpaka nikafika mahali ambapo ningeweza kushuka na kujinunulia sambusa, nami nikachukua kifurushi chake na kurudi kwenye garimoshi, mnaona, nami ni—ningeweza—ningeweza kuishi kwa hiyo. Kwa hiyo basi, nikanunua . . . nisingeweza . . . Siamini katika kuchukua pesa za watakatifu na kuzitumia, kwa vitu kama hivyo.

²¹⁶ Kwa hiyo basi, ni—nikachukua, nikajinunulia sambusa, nami nilikuwa nikishuka kule, nikikimbia *huku* chini kuelekea mahali stendi ilipokuwa, nikamsikia mtu fulani akisema, “Halo hapo, Kasisi Branham!” Nikaangalia pande zote, maskini mbeba mizigo.

Nami nikasema, “Halo hapo.”

Akasema, “Ngoja kidogo!” Akaja pale, akasema, “U hali gani?”

Nami nikasema, “Ni—niko salama.” Nikasema, “Siamini ninakujua.”

Akasema, “Loo, naam, unanijua.”

Nami nikasema, “Mimi. . . labda nimekusahau tu.”

Kasema, “Unakumbuka ukishuka kuja barabarani asubuhi moja, na kuja kwenye nyumba ambamo mvulana mmoja alikuwa amelala, akifa kwa ugonjwa wa zinaa?”

Nikasema, “Wewe siye. . . !”

Kasema, “Naam, bwana, *mimi ni yeye.*” Akasema, “Mimi sikupona tu, bali *mimi* ameokoka sasa, Kasisi Branham.”

²¹⁷ Loo, nusu haijasimuliwa bado. Baba mwema wa Mbinguni, mwenye rehema, wa thamani, anaweza kufanya nini cha zaidi ku—kutuonya, na kutuweka sawa? Anaweza kufanya nini zaidi? Mnampenda? Je, unampenda kwa moyo wako wote, nafsi yako yote, na kwa akili zako zote?

²¹⁸ Ni wenye dhambi wangapi walio hapa ndani sasa? Tunapoinamisha vichwa vyetu, kwa muda kidogo tu. Inua mkono wako, useme, “Mungu, weka Moto katika taa yangu usiku wa leo, Bwana. Washa mshumaa wangu mdogo na uniache niwake kwa ajili ya Kristo mpaka nitakapokufa.” Sema, “Sasa ninashika njia yangu pamoja na wachache wa Bwana waliodharauliwa.” Hebu nione mkono wako. Rafiki mwenye dhambi, waweza kuinua mkono wako, umkubali Kristo kama Mwokozi wako? Waweza tu kuinua mkono wako, roshani, au orofa ya chini?

²¹⁹ Tumelichambua kila usiku. Labda kulikuwa na mwingine mmoja ama wawili hapa usiku wa leo, inua mkono wako, utafanya hivyo? Mahali popote, mwenye dhambi? Sema, “Na—nataka kumpokea Roho Mtakatifu.” Sasa kumbuka, ama utakuwa na Roho Mtakatifu, au utachukua alama ya mnyama, kuna matabaka mawili tu. Tatalifikia kesho usiku. Kwa namna fulani nililitupa tu nje, na kufanya msingi mkubwa wa kulimalizia kesho usiku.

²²⁰ Inua mkono wako, useme, “Ninamtaka, Ndugu Branham.” Mungu akubariki, kijana, Bwana akubariki, hilo ni zuri sana. Mungu akupe shauku ya moyo wako, mwanangu. Mtu mwingine, angesimama tu, aseme, “Ninataka kumkubali Kristo.” Mungu akubariki, mama. Hilo ni zuri sana, jambo la kishujaa sana. Mtu mwingine asimame, aseme, “Nitamkubali Kristo, nitampokea.” Kwenye roshani? Huko nyuma kabisa pembeni, naam. Mimi, bwana, ninauona mkono wako huko juu, rafiki yangu mpendwa. Sasa, mtu mwingine aseme, “Hebu mimi. . .” Hebu tuone sasa, mtu mwingine aseme, “Nitamkubali Kristo kama Mwokozi wangu. Nitamwinulia mkono wangu na kusema, mimi. . .”

²²¹ Sasa, unakumbuka, unapoinua mkono wako, unamaanisha, hilo latosha, limetendeka milele. Mungu anakuchukulia

kwa neno lako. Limaanishe tu, inua mkono wako, uone kitakachotukia.

222 Vema, mwingine huko juu kwenye roshani, Mungu akubariki. Naam, hilo ni zuri. Inua tu mkono wako, uone ni hisia ya namna gani inayokujia. Kama wewe ni mwenye dhambi inua mkono wako. Naam, huyo mama, msichana aliyeketi hapa mbele, Mungu akubariki, Dada, mpendwa. Mwingine? Nitakuwa nikingojea, Kristo anangojea. Mungu awabariki huko juu. Mwingine? Mungu akubariki huko nyuma, ewe jamaa mdogo. Mungu awe pamoja nawe, mwanangu. Kwa hiyo, Mungu hakika atafanya hivyo.

223 “Ninataka kumkubali Kristo kama Mwokozi wangu.” Mungu akubariki, huko nyuma. Mwingine? “Nitamkubali Kristo kama Mwokozi wangu. Mimi sasa, mahali hapa, ninapoketi, nimeshawishika ya kwamba ninamhitaji Kristo. Ninajua hilo, daima nimeamini ya kwamba unakuja wakati wa utengano, ambapo Mungu angelitenganisha Kanisa la kweli.” Yeye ataninii, atalipeleka Nyumbani, analitayarisha sasa hivi.

224 Je, utakuja kujiunga na Yesu Kristo kwa kumpa Yeye moyo wako? Endelea tu kanisani popote ulipo, endelea tu, lakini mpe moyo wako. Inua . . .

225 Sasa, madhehebu, wao ni, moja ni kama tu hayo mengine. Ni, popote pale, popote ulipo na ushirika wako, kundi la watu unaowapenda, hilo ni sawa. Kama wewe ni mfuasi wa Foursquare, usigeuke kuwa Assemblies; kama wewe ni mfuasi wa Assemblies, usigeuke kuwa Foursquare, kaa tu mahali ulipo na umpende Bwana, popote ulipo. Ume—umebatizwa katika Mwili wa Kristo, kwa hiyo dhehebu lolote ulilo mfuasi wake, halikuokoi, wala halina uhusiano wowote nao, ni mahali tu ambapo watu huja. Na ndugu halisi, wa kweli wanajua hilo, sote tunajua hilo, tunajua hilo, bila shaka, tunajua.

226 Hivi wewe . . . ? Kuna mwingine atakayeinua mkono wake kabla hatujaomba? Mungu akubariki, kipenzi. Kunaweza kuwa na mwingine? Inua mkono wako, useme, “Mimi—mimi, juu ya msingi wa Damu iliyomwagika, kile Yesu alichonifanyia . . . Na Ndugu Branham, yale nimekusikia ukisema usiku wa leo, siamini ya kwamba ungetwambia jambo lolote lisilo sahihi, bila shaka ninaamini ya kwamba wewe ni mtumishi wa Mungu. Na juu ya ujumbe kwamba ‘Imani yako chanzo chake ni kusikia, kusikia Neno la Mungu . . .’”

227 Tutaingilia jambo hilo kwa utamu sana kesho usiku, wakati tukimalizia ubatizo wa Roho Mtakatifu na alama ya mnyama.

228 Utainua mkono wako? Useme, “Juu ya msingi wa Damu ya Kristo iliyomwagika, ninamwinulia mkono wangu, nikisema, ‘Nataka uwe Mwokozi wangu sasa hivi.’” Je, kuna wengine zaidi, kabla hatujaomba?

229 Mungu akubariki, ewe msichana, huko nyuma, hilo ni zuri sana. Mungu awe pamoja nawe, dada yangu. Kunaweza kuwa na mwingine? Mungu akubariki, dada yangu, uliyeketi papa hapa, hilo ni zuri sana. Kunaweza kuwa na mwingine? Huko nyuma kabisa, Mungu akubariki, ndugu yangu, hilo linaleta tofauti kati ya mauti na uzima.

230 Sasa, nini, wewe uliyeinua mkono wako, vipi kama usiku wa leo ulikuwa usiku wako wa mwisho duniani? Na kama wakati fulani kati ya sasa na mchana, ungeamka katika usingizi wako, na moyo wako unasimama, mishipa ya—yako inapoa, mikono yako inaingia baridi, unabonyeza m—mto wakati ukifa, daktari anaondoka mlangoni akasema, “La, ni mshtuko wa moyo, wameondoka,” mnaona, hakuna kitu... ulimsikia akisema hivyo? Si litakuwa jambo zuri sana unapojua ya kwamba uliinua mkono wako? Loo, ni tamu jinsi gani! Jinsi utakavyokuwa na furaha!

231 Vipi kama ukipata ajali ukienda nyumbani, nawe umelala kando ya barabara, ukitokwa na damu, ukisikia gari la kuchukulia wagonjwa likija, lakini unajua limechelewa kupita kiasi, nawe unajua ya kwamba ulimwinulia Kristo mkono wako? Ungesema, “Na iwe, sina budi kwenda wakati fulani, kwa vyovyote vile, kwa hiyo niko tayari sasa, na sasa ndio wakati wa kuondoka.”

Inua tu mkono wako. Fanya uamuzi huo mmoja wa yote sasa hivi, je, utafanya hivyo, ndugu yangu, dada yangu? Inua mkono wako.

Unasema, “Ndugu Branham, mbona unawasihi watu hivyo? Hii si maskani yako, hili si kanisa lako.”

232 Najua. Ndugu Buntain, ndugu yangu, ndiye mchungaji hapa. Assemblies of God, kanisa hili ni lao, ambalo, jengo hili hapa, nao Assemblies of God ni mojawapo ya wadhamini wangu mashuhuri sana katika milki za Kipentekoste kote ulimwenguni, hiyo siyo, lakini bado, wote hao, kadiri ninavyowapenda, hiyo siyo sababu, ninawapenda, nawapenda kama mtu binafsi, sitaki mpotee.

233 Nilipata ono, natumaini nitapata wakati wa kuwasimulia, yaliyotukia, siku chache zilizopita usiku, niliuona Utukufu, na kuona watu, nikaona mwanamke akikimbia na kunikumbatia kwa mkono wake kule juu. Nimekuwa mkali kidogo kwa wanawake, kwa vyovyote vile, nami nikamwona mwanamke huyo, kitu cha kupendeza sana nilichopata kuona. Naye akaniita ndugu yake mpendwa.

Nami nikasema, “Kwa nini akafanya hivyo?”

Kasema, “Alikuwa amepita umri wa miaka tisini ulipomwongoza kwa Kristo.”

Nikasema, “Ee Mungu, laiti ningaliweza kurudi, nitashawishi, nitaomba, nitasihi, nitafanya kila kitu.”

²³⁴ Hivi hutainua mkono wako, na kusema, “Ninamkubali Kristo kama Mwokozi wangu”? Hakika, Mungu akiniruhusu kufanya yale ninayomfanyia, hakika najua, nina wazo la jinsi—jinsi ya kumpokea Yeye.

²³⁵ Kunaweza kuwa na mshiriki vuguvugu wa kanisa hapa? Sasa, kila mtu ukiwa umeinamisha kichwa chako. Mshiriki vuguvugu wa kanisa, ninii tu, umekiri kwamba ulimjua Kristo, lakini kwa kweli, ndani ya moyo wako hujamjua, bali unataka kumjua Yeye, inua mkono wako, mshiriki wa kanisa. Mungu akubariki, bwana. Mwingine? Mungu akubariki, Ndugu. Mungu akubariki.

²³⁶ Mtu mwingine, mfuasi tu wa kanisa, aseme, “Ninataka kumjua Kristo, mimi—mimi ni mfuasi wa kanisa.” Na si—siwezi kusema neno baya dhidi ya hilo. Hakika afadhali niwe kwenye. . . kuwa mfuasi wa kanisa, kuliko kuwa huku nje mtaani bila chochote. Nenda kanisani, bali ninakutaka, tafadhali njoo upokee Muhuri wa Mungu.

²³⁷ Maana, kama huna, vema Biblia inasema kuna matabaka mawili tu. Ngojeni mpaka kesho usiku, nanyi mtaona. Matabaka mawili, moja litakuwa na alama ya mnyama, lingine litakuwa na Muhuri wa Mungu. Kama tu vile Kaini na Sethi katika bustani ya Edeni, wanakifikia kitu hicho. Je, uta—utainua mkono wako? Mmoja zaidi sasa, kabla hatujaomba. Mungu akubariki, mama.

²³⁸ Baba yetu wa Mbinguni, nimeona mikono mingi ikiinuliwa usiku wa leo, wengi wao ni wenye dhambi nao wanataka msamaha wa dhambi. Wawili waliinua mikono yao kwamba walikuwa tu washiriki wa kanisa, na hata hivyo hawakukujua Wewe, wala hawakuwa wametiwa muhuri kuingia katika Ufalme.

²³⁹ Baba, ni—ninaleta Maandiko haya, na kuyaweka mbele Zako, Ulisema katika Neno Lako, “Yeye alisikiaye Neno Langu,” na Bwana, kadri nijuavyo mimi, nimelihubiri, “na kumwamini Yeye aliyenipeleka, yuna Uzima wa Milele.” Sasa, Wewe ulisema hivyo, Baba, hivyo ndivyo hasa ulivyosema, nami ninayarudisha moja kwa moja kwenye kumbukumbu Yako. Watu hawa wamelisikia Neno hilo, nao wamemwamini Yeye aliyekutuma.

²⁴⁰ Sasa, Wewe ulisema, “Wanao sasa,” wakati uliopo, *wanao*, wakati uliopo, “Uzima wa Milele, wala hataingia Hukumuni, bali amepita kutoka mautini kuingia Uzimani.” Walifanya jambo hilo lini? Walipoinua mkono wao, waliposema waliamini. Sasa, Bwana, Wewe ulisema hilo, nami ninawadai watu hao.

²⁴¹ Shetani, huwezi kuwashikilia, hata hivyo, tena, wao ni watoto wa Mungu sasa hivi. Ninaleta hilo mbele zenu. Inakubidi kuondoa mkono wako maishani mwao, wao ni wa Mungu sasa.

Ninawadai kwa ajili Yake, ninawadai kama nyara za—za upendo wa Kristo pale Kalvari. Ni—ninakupaa changamoto katika mjadala, huna mamlaka yoyote ya kisheria, huna mamlaka juu yao, hukuwa nayo kwanza kabisa, ulikuwa tu ukiwahadaa, ulikuwa tu ukihadaa. Kristo alikuvua kila kitu ulichokuwa nacho pale Kalvari, akavua kila nguvu ulizowahi kuwa nazo, nawe si kitu ila laghai, nasi tunaupa ulaghai wako changamoto. Hawa ni watoto wa Mungu sasa.

²⁴² Na Baba, Wewe ulisema, “Yeye atakayekuja Kwangu, sitamtupa nje kamwe,” Uliahidi jambo hilo, nami ninajua ni kweli. Ulisema ungewapa Uzima wa Milele na kuwafufua katika siku ya mwisho, basi wana hakika kuja katika ule ufufuo kadiri wanavyoketi katika jengo hili usiku wa leo.

²⁴³ Sasa, Baba, ninauliza tu jambo moja zaidi: Je, utawajaza na Roho Mtakatifu? Tujalie hilo, Bwana. Loo, wajaze na Roho Mtakatifu. Usiache—usiache nafsi yao istarehe, Bwana. Jalia usiku kucha, mito yao iwe migumu, jalia iwe migumu kama mawe, kitanda chao, hata wawe huko nje wamepiga magoti, wakisema, “Mungu, nijaze na Roho Mtakatifu.” Jalia waichukue Biblia, waisome, pia naomba Wewe uje kwao na kuwafasiria Neno, na jalia wasiwe na starehe sasa. Wao ni watoto Wako, na saa inaenda sana, ninaomba ya kwamba watapata amani hiyo ipitayo akili zote, kwa Yesu Kristo.

²⁴⁴ Hawa washiriki wa kanisa walioinua mkono wao, Baba, ninakushukuru kwa ajili yao. Wao—wao—wao wamekiri na kuingia kanisani, bali wanatambua kuwa tu mfuasi wa kanisa, wangetiwa alama kama aina mbaya ya mwanamke. Tatalifikia hilo kesho usiku, kama ukitaka, Baba, waonyeshe jinsi walivyotiwa alama kama bibi-arusi wa uongo. Bibi-arusi wa kweli ana Mafuta katika taa zao. Ninaomba, Baba, ya kwamba utawapa Mafuta katika taa yao, usiku wa leo. Jalia hao washiriki wa kanisa wajazwe na Roho Mtakatifu usiku wa leo. Tujalie, Bwana.

²⁴⁵ Ninaomba jambo hili, si kwamba niwe mwovu, bali niwe ndugu yao, tukijua ya kwamba kukosa Mbingu ni kukosa yote. Maskini muda huu mdogo wa maisha ni nini, ukilinganishwa na Umilele ulivyo? Unayeyuka tu ukawa u—usio na mwisho, kwa sababu kamwe haukuanza. Na, Baba, ninaomba ya kwamba utawavuta juu katika siku za mwisho katika milki hizo za Milele za Utukufu pamoja Nawe. Tujalie, hao ni Wako. Ninaomba, na kuwakabidhi Kwako, katika Jina la Kristo.

²⁴⁶ Sasa, huku vichwa vyetu vimeinamishwa, nitamwomba kila mmoja aliyeinua mikono yao, wasimame tu kwa miguu yao. Sitawaomba mje huku juu, hatuna nafasi yoyote. Lakini nyote mlioinua mikono yenu, kama wewe ni mwaminifu kwa Mungu, simameni tu kwa miguu yenu, kwa muda kidogo tu. Kila mtu aliyeinua mkono wake, simama kwa miguu yako, kila mahali,

kwenye roshani, kila mahali, simama tu. Yesu alisema, “Yeye atakayenikiri mbele ya watu, huyo nitamkiri mbele za Baba Yangu na Malaika watakatifu.”

²⁴⁷ Sasa, ninawatakeni ninyi washiriki wa kanisa, na ninyi Wakristo, hasa, kuangalia kila mahali, mwone hao ni akina nani. Ninawatakeni mshike mkono wao, na kuwapa mkono, msimame hapo, msemi, “Mungu akubariki. Karibu katika Ufalme wa Mungu, Msafiri.” Jambo ndilo hilo, mgeukie mtu fulani moja kwa moja, peaneni mikono nao, ukisema, “Karibu katika Ufalme wa Mungu.” Hilo ni zuri sana. Hilo ni zuri sana. Hilo ni zuri. Mungu awabariki. Bwana awe pamoja nanyi. Hilo ni zuri sana. Vema. Mungu awabariki.

Sasa, mnaweza kuketi. Hilo ni zuri sana, sana.

²⁴⁸ Sasa, nitawaomba mfanye jambo fulani sasa: Hakikisha utampata mchungaji mmoja, kama hujawahi kubatizwa katika ubatizo wa Kikristo, tafuta mchungaji fulani, ujichagulie kanisa, kisha ubatizwe katika maji, katika ushirika wa kanisa hilo. Halafu ukifanya hivyo, ndipo uatafute ubatizo wa Roho Mtakatifu mpaka umejazwa na Roho Mtakatifu, na:

Nitakutana nawe asubuhi, kando ya mto
mwangavu,
Wakati huzuni zote zimetoweka;
Nitakuwa nimesimama langoni, wakati
malango yatakapofunguliwa wazi,
Mwishoni mwa siku ndefu ya maisha yenye
uchovu.

Nitakutana nawe asubuhi na “U hali gani,”
Nasi tutaketi kando ya mto na kufanya upya
urafiki wa kale tukiisha kunyakuliwa,
Utanjua asubuhi, kwa tabasamu nililo nalo,
Nitakutana nawe asubuhi, katika Mji, Mji
uliojengwa miraba minne.

²⁴⁹ Baba Mungu, wao ni Wako sasa, wametiwa muhuri katika Ufalme wa Mungu, Roho Mtakatifu akiwashughulikia. Sasa naomba ya kwamba wataninii... Nitakutana nao asubuhi kwenye ile Pwani angavu, inayometameta, ng'ambo, wakati huzuni zote zimetoweka. Si itakuwa ni ajabu, Baba? Kengele za furaha zikilia, mioyo yote ikichangamka, ikiimba, utakuwa ni wakati mzuri sana. Wao ni Wako, nami ninaomba ya kwamba utawaweka kwa neema Yako, mpaka tutakapokutana kwenye mto huo, asubuhi hiyo. Amina.

Sasa, hivi hujisikii vizuri? Si inakufanya ujisikie vizuri sana? Sema, “Ndugu Branham...”

²⁵⁰ Waongofu vijana sasa ambao ndio kwanza waingie katika Ufalme, nitamwomba Baba kama atafanya jambo fulani, nina haki ya kumwomba sasa, wenye dhambi walikuja, ninaamini tunapata kibali Kwake, sivyo?

²⁵¹ Ni wangapi walio wagonjwa huko nje? Inueni mikono yenu, wagonjwa tu na wahitaji. Vema. Nitageuza mgongo wangu kuwaonyesha ya kwamba tuko katika siku ya mwisho. Ni wangapi wanaokumbuka masomo yetu? Jinsi Malaika wa Bwana, Mungu, alivyoshuka na kukaa katika mwili wa mwanadamu, na kula nyama, mwanadamu wa kawaida tu, akinena hivyo, na hata hivyo Mungu alikuwa katika mwili wa mwanadamu kabla tu ya Sodoma kuteketezwa. Naye Yesu alisema ishara ya namna ile ile ingetukia wakati wa kuja kwa Mwana wa Adamu. Tunaamini hilo? Jinsi ambavyo tumepitia kwenye masomo kuonyesha yale aliyofanya.

²⁵² Sasa, hakuna mtu hapa ninayemjua. Ninaamini nilikuwa nikiwinda majuma machache yaliyopita pamoja na kijana huyu aliyeketi papa *hapa*. Hivi wewe si una uhusiano fulani na rafiki yangu mwema? Si...? Wewe ni shemeji ya Ndugu Norman, naamini hiyo ni kweli, sivyo? Vema. Huyu ndiye mtu pekee, na Ndugu na Dada Smith walioketi hapa, Ndugu Gene, na hao tu ndio ninaowajua, nitageuka...na, naam, Dada Upshaw, nakutakia heri, Dada Upshaw.

²⁵³ Loo, jinsi ninavyompenda Ndugu Willy Upshaw! Mkutano wenu usiku ule, Ndugu Kopp, nilipoangalia pale na kuona, nilikuwa nikijaribu kuzungumza, kisha nikamwona mahali alipoanguka kutoka kwenye mkokoteni huo, akaumiza mgongo wake, nao wakaona wasingeweza kumfanyia chochote. Sijawahi kusikia habari zake maishani mwangu. Naye huyo hapo, Willy D. Upshaw. Nikasema, “Vipi...?”

Ern alinijia, kasema, “Vipi kuhusu mtu yule?”

²⁵⁴ Nikasema, “Amegombea urais wakati mmoja na angeshinda huo uchaguzi, kama isingalikuwa ni msimamo wake dhidi ya wiski na kitu kibaya. Chama cha Demokrasia kingemchagua. Lakini a—alichukua msimamo wake.” Ndipo nikasema, “Miaka hii yote, miaka sitini na sita, umekuwa kwenye haya magongo na kiti cha magurudumu, lakini Mungu anamwondoa humo sasa.” Huyu hapo, na jinsi alivyo mtamu!

²⁵⁵ Nitakapofika Ng’ambo ya pili nitamwona kijana, mwenye sura nzuri akishuka na kusema, “Unanikumbuka, Ndugu Branham? Mimi ni Ndugu Upshaw.”

²⁵⁶ Nimwone maskini mpenzi wake pale, wote pamoja. Ninakumbuka jinsi ulivyolia usiku huo, Dada Upshaw, ulipomwona akisimama, akakimbia jukwaani, na kugusa vidole vyake vya miguu kwa mkono wake akiwa na umri wa kama miaka themanini. Jamani, jinsi Mungu anavyoweza kufanya mambo makuu!

²⁵⁷ Vema. Malaika wa Bwana aliketi huku amegeuza mgongo Wake. Sasa, sasa, natumaini nyote mtalipata hili, mimi si Malaika wa Bwana, mimi ni William Branham. Mnaona? Mimi ni ndugu yenu. Lakini Yeye alikuwa akiishi katika mwili wa

mwanadamu wakati huo ambao alijiumba Mwenyewe, kisha akatoweka tu. Mnaamini hilo? Sasa, mnaamini huyo alikuwa ni Mungu? Biblia ilisema ilikuwa ni Mungu, Ibrahimu alisema ilikuwa hivyo.

²⁵⁸ Ilikuwa ni kitu gani? Ishara kwamba katika siku za mwisho... Sasa mnakumbuka, wakati alipokuja katika siku za Bwana Yesu, Yeye, Mungu aliishi ndani ya Yesu, hivi humwamini hilo? Huo ulikuwa ni mwili uliozaliwa na bikira, Mbegu iliyotoka kwa Mungu, Mwenyewe. Na katika Chembe hiyo ya Damu, ilipovunjwa pale Kalvari kwa ajili ya dhambi zetu, ndipo ikalitakasa Kanisa, kusudi Roho Mtakatifu apate kukaa ndani ya Kanisa na kuendeleza kazi za Mungu. “Ninyi ni mashahidi Wangu, mkiisha kupokea nguvu.” Hiyo ni kweli.

²⁵⁹ Sasa, kama hili, kama nimesema kweli, basi hebu Roho Mtakatifu aseme nawe usiku wa leo. Nitageuza mgongo wangu, ninyi ombeni, angalieni kama ni Roho Mtakatifu yeye yule. Sasa, Yeye hana budi kufanya kazi pamoja nanyi kama vile anavyofanya kazi pamoja nami.

²⁶⁰ Baadhi yenu ndugu hapa nje waombeeni wale walio huko nje kwenye kusanyiko, wahudumu, na kadhalika. Tutakuwa na wakati, wahudumu.

²⁶¹ Baba wa Mbinguni anajua ya kwamba sifanyi hivi kwa kusudi lingine, bali kwamba Ne—Neno ninalohubiri lipate kudhihirishwa kwa Kanisa katika siku hii, ambapo kanisa la Kipentekoste limemwacha Mungu, halina budi kurudi. Ni wakati wa Laodikia.

²⁶² Pia, Mungu, kama nimesema jambo lolote dhidi ya mtu yeyote la kumdhuru ambalo hukuniambia Wewe, nisamehe, Bwana, bali nililifanya jinsi tu ulivyonipa. Kwa hiyo ninaomba, Baba, ya kwamba Wewe utathibitisha. Nilinena habari Zako, sasa nena ya kwamba nilisema kweli, Bwana. Ninalikabidhi Kwako, katika Jina la Bwana Yesu.

²⁶³ Kuna mamia kadhaa ya watu walioketi hapo, wengi wao ni wagonjwa, sijui hata mmoja wao, Wewe unawajua, ninaomba ya kwamba utalitimiza Neno Lako. Wakati ulipokuja hapa duniani, ulisema ya kwamba ulifanya hivyo ili litimie, ambalo lilinenwa na nabii Isaya, kile Masihi angefanya. Sasa, Baba, jalia litimie tena, kwa kuwa Wewe uliliahidi, hiyo ndiyo sababu unaliruhusu. Katika Jina la Kristo. Amina.

Sasa, kuna wengi wanaoomba. Kama ninaweza... Ikiwa mtu fulani, kama maskini yule mwanamke, angeweza kugusa vazi Lake!

²⁶⁴ Naam, moja kwa moja mbele yangu sasa linakuja ono, na inatokea kwamba ni mwanamke, ameketi, jinsi ninavyosimama sasa, angekuwa mkono wangu wa kulia, upande huu. Anaogua ugonjwa wa kibofu nyongo, ana ugonjwa wa moyo pia. Huku

nimegeuza mgongo wangu, kama nikilitaja jina lake, labda angeelewa. Bibi Hanson, simama na upokee uponyaji wako.

Sasa, sijawahi kuangalia kote, bado. Sasa, mnaamini? Iweni tu na imani. Huyu mama alikuwa wapi? Amerudi huku mahali fulani. Papo hapo?

Je, mambo hayo yalikuwa ni kweli, mama? Hivi hatufahamiani? Kama ndivyo, pungu mkono wako namna *hii*. Yote yalikuwa ni kweli, sivyo?

²⁶⁵ Basi Malaika yule yule wa Mungu aliyekuwa ameketi kule Sodoma, Gomora kumpa Ibrahimu ishara kwamba saa ya kuteketezwa kwa Sodoma ilikuwa inakaribia, yuko hapa usiku wa leo. Karama tu ya kujituliza.

²⁶⁶ Ninamwona juu ya mtu mwingine. Natumaini... (Sasa, msiniache nikae sana.) Ninaangalia tu ono, mwanamke aliyeketi hapa akiomba. Ana kisukari. Bibi Finch, unaamini ya kwamba Mungu atakuponya? Kama unaamini, simama, inua mkono wako. Sikujui, hiyo ni kweli? Kama hiyo ni kweli, pungu mkono wako. Je, hiyo ndiyo shida yako? Yale Yeye...? Vema. Uligusa kitu Fulani, sivyo? Kile...? Hukunigusa mimi, sivyo? Ulimgusa—ulimgusa Mungu, hiyo ni kweli. Mungu akubariki.

²⁶⁷ Unafikiri nini kijana, unayesugua pua yako? Unamhitaji Mungu, pia. Unaamini? Mungu atanielezea shida yako ni nini. Huna kadi ya maombi, nadhani, la, hakuna, hiyo ni kweli, hakuna kadi ya maombi. U—unaniamini mimi kuwa ni nabii Wake? Ama, mtumishi Wake, ninakusudia kusema. Samahani kwa kusema hivyo, mimi si nabii, mimi ni mtumishi Wake tu.

²⁶⁸ Unasumbuliwa na wasiwasi, wasiwasi sana hata huwezi kujishikilia pamoja. Hiyo si ni kweli? Kama hiyo ni kweli, inua mkono wako. Unaamini yale ningesema yangetimia? Unaamini? Utanitii mimi kama nabii Wake? Basi ninaondoa wasiwasi huo kutoka kwako, katika Jina la Yesu Kristo. Kamwe usizungumze juu yake tena. Nenda ukaponywe.

²⁶⁹ Hivi Bwana wetu hakusema, “Ukiuambia mlima huu, ‘Ng’oka’”? Kama unaweza kuamini!

²⁷⁰ Mtu aliyeketi papo hapo nyuma akiniangalia, angetaka kuja hapa, anataka nimwekee mikono. Hiyo ni kweli. Huko kukakamaa kwa ateri kungekuacha kama tu ungeamini papo hapo unapoketi. Utafanya hivyo? Uliyeketi moja kwa moja huko nyuma, kidogo una mvi, umevaa miwani, umeketi papo hapo nyuma ukiniangalia. Kama utaamini kwa moyo wako wote! Usitie shaka. Unaamini?

Sasa angalia, alizunguka moja kwa moja kutoka kwa mtu huyo, aliupoteza.

²⁷¹ Unasugua macho yako, kisha ukageuka, na kuangalia kwa maskini... Jambo ndilo hilo. Mama huyu aliyeketi papa hapa, iko moja kwa moja juu yako uliye na ugonjwa wa moyo, uliyeketi

hapo. Unaamini ya kwamba Mungu atakuponya? Papo hapo. Naam. Vema. Pokea uponyaji, ni wako. Vema. Mungu awabariki.

Iweni macho, mwe tayari kulishika dakika yoyote.

²⁷² Mtu mzuri sana, una imani nyingi, una mawasiliano mazuri na Mungu. Sikujui. Lakini unaamini ya kwamba Mungu ataponya ugonjwa huo wa moyo ulio nao, pia? Una tatizo la mguu wako, pia, hivi huna ninii, kiungo chako? Naam, una binti ambaye hajaokoka, unayemwombea. Hiyo ni kweli. Wewe hutoki hapa, unatoka Hollywood ya Kaskazini. Unajua ninazungumzia nani sasa? Unataka nilitaje jina lako? Bibi Beard, simama kwa miguu yako, na uukubali, katika Jina la Yesu Kristo.

Unaamini? Sasa, ni nini, marafiki?

Je, mambo hayo ni ya kweli, mama? Kama ndivyo, pungu mkono wako.

Mnaona, ni kweli. Mnaona? Sasa, mnaamini? Sijawahi kumwona mwanamke huyo maishani mwangu. Sasa angalieni, jengo lote. . .

Sasa, wa—walinigusa, mnaona, ninajua imetosha tu sasa. Wao huniangalia, mwajua, ninapofanya ya kutosha.

²⁷³ Sasa, hebu nikwambie, rafiki yangu, nimekwambia kweli, Mungu amethibitisha ya kwamba nimekwambia kweli. Upako ule ule wa Mungu unaohubiri Neno lili na kusema mambo haya, ndio upako wenyewe unaotangaza ya kwamba Mungu yupo hapa, akifanya jambo lile lile. Unaamini kwa moyo wako wote?

Ni wangapi wenu wanataka kumpokea Roho Mtakatifu? Inua mkono wako, useme, “Ningependa kumpokea Roho Mtakatifu.”

²⁷⁴ Mchungaji ananiambia kuna chumba moja kwa moja *pale* chini, kinangojea tu mtu fulani ashuke aje, aingie apate kuombewa. Kwa nini msiupokee? Shukeni mwende kule m—mkampokee Roho Mtakatifu.

Hebu sote tusimame kwa miguu yetu, wakati mmoja. Hebu tuinue mikono yetu, na kumpa Mungu sifa, kila mtu, kwa njia yako mwenyewe. Usininii. . . Amini tu.

²⁷⁵ Baba wa Mbinguni, ninakupa sifa na utukufu, kwa matendo yote makuu, kwa mambo yote ambayo umefanya. Wewe ndiwe Mungu asiyeokosea, Wewe Ndiwe yeye yule jana, leo, na hata milele, Wewe hushindwi kamwe.

²⁷⁶ Sasa, wekeaneni mikono, wekeaneni mikono mpate kuponywa, na kumpokea Roho Mtakatifu. Sasa, mwombee mtu huyo, ombeaneni. Huko juu kwenye roshani, huko juu, wekeaneni mikono, ombeaneni, mpate kumpokea Roho Mtakatifu. Kama hamtatilia shaka, Mungu atampa kila mmoja wenu ubatizo wa Roho Mtakatifu, na atamponya kila mmoja.



61-0216 Alama Ya Mnyama Na Muhuri Wa Mungu #1
First Assembly Of God Of Long Beach
Long Beach, California Marekani

SWAHILI

©2025 VGR, ALL RIGHTS RESERVED

VOICE OF GOD RECORDINGS
P.O. Box 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.
www.branham.org

Ilani ya haki ya kunakili

Haki zote zimehifadhiwa. Kitabu hiki kinaweza kuchapishwa kwa matbaa ya nyumbani kwa matumizi ya kibinafsi ama kusambaza, bila malipo, kama chombo cha kuitangazia Injili ya Yesu Kristo. Kitabu hiki hakiwezi kikauzwa, kunakiliwa kwa wingi, kuwekwa kwenye mtandao, kuhifadhiwa kikatolewe tena, kufasiriwa katika lugha zingine ama kutumiwa kuomba fedha bila idhini halisi iliyoandikwa moja kwa moja kutoka Voice Of God Recordings®.

Kwa habari zaidi ama kwa vifaa zaidi, tafadhali wasiliana na:

VOICE OF GOD RECORDINGS

P.O. BOX 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.

www.branham.org